BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,012,798,111/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Muuguzi** aliyeomba rushwa, adaiwa kukutwa na gongo

UKURASA 7

Nipashe
Ijumaa Julai 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581000 *
www.ippmedia.com
The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710 LIKE & FOLLOW



STERLING ATHIBITISHA KUONDOKA MAN CITY

UKURASA 21

# Wakuu wa mikoa watapeliwa viwanja

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### TAMISEMI YATOA HADHARI WANAOKULA FEDHA MBICHI

OFISI ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imesema katika mwaka huu wa fedha, haitavumilia wala kumwonea...

## Kibano maduka ya dawa nje ya hospitali chaja

UKURASA 2



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiangalia vitabu mbalimbali katika mabanda ya walioshiriki maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Sauda Msemo (wa pili kushoto), akikata utepe ili kuzindua tawi la NMB Buhongwa, jijini Mwanza juzi. Wengine ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi (wa tatu kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi (kushoto), Mbunge wa Nyamagana, Stanslaus Mabula (kulia), Meya wa Jiji la Mwanza, Sima Costantine (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




## Tanzania na Afrika Kusini zaingia ubia ajira lugha Kiswahili

UKURASA 4

MICHEZO YANGA YAANZA HESABU ZA CAF UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Asilimia 97 Watanzania wako tayari kuhesabiwa

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, amesema tathmini iliyofanywa hivi karibuni na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), imebaini asilimia 97 ya Watanzania wako tayari kuhesabiwa.

Vilevile, idadi hiyo ni zaidi ya ile iliyokuwapo katika sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 ambapo asilimia 80 ya Watanzania ndiyo walikuwa tayari kuhesabiwa katika kipindi kama hicho.

Dk. Chuwa alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kuanza kwa mafunzo ya wakufunzi wa sensa ya watu na makazi ngazi ya mkoa.

Alisema hali hiyo inatokana na mwitikio mkubwa uliopo katika jamii kutokana na elimu ambayo imekuwa ikitolewa kwa jamii kupitia njia mbalimbali ikiwamo vyombo vya habari.

Mtakwimu huyo alisema hadi sasa tayari wameshatoa elimu kwa makundi mbalimbali katika jamii ikiwamo wahariri wa vyombo vya habari ili kuuelimisha umma kuhusu umuhimu wa sensa.

"Tathmini ambayo tumefanya inaonyesha kuwa takribani asilimia 97 ya Watanzania mpaka sasa wapo tayari kuhesabiwa kulinganisha asilimia 80 ya Watanzania iliyokuwapo wakati kama huu katika sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012," alisema Dk. Chuwa.

Akizungumzia kuhusu mafunzo kwa wakufunzi wa sensa ya watu na makazi 2022, Dk. Chuwa alisema kwa ngazi ya taifa yamekamilika, yakifanyika kwa siku 21 kuanzia tarehe 10 hadi 30 Juni mwaka huu.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo na uelewa wa pamoja washiriki wote kuhusu nyenzo zote za sensa pamoja na utaratibu mzima wa kufanya sensa ya watu na makazi, sensa ya majengo na sensa ya anwani za makazi ili waweze kwenda kufundisha katika ngazi za mkoa.

Alisema washiriki wa mafunzo katika ngazi ya taifa walikuwa wataalamu kutoka katika wizara, idara na taasisi za serikali, wawakilishi kutoka vyama vya watu kwenye ulemavu na wawakilishi kutoka sekta binafsi na vyuo vikuu.

Mtakwimu huyo alisema hatua inayofuata ni mafunzo katika ngazi ya mkoa ambayo yameanza rasmi juzi katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

"Mafunzo haya yatafanyika kwa siku 21 kuanzia tarehe 6 hadi 26 Julai, 2022, washiriki wakiwa ni wataalamu kutoka TAMISEMI ikiwa ni pamoja waratibu wa sensa wa wilaya, maofisa elimu mkoa na wilaya, wataalamu wa TEHAMA wa wilaya, maofisa maendeleo ya jamii wa wilaya, maofisa mipango wa wilaya, waratibu elimu kata pamoja na wawakilishi kutoka vyama vya watu kwenye ulemavu nchini," alisema.

Dk. Chuwa alisema kuwa baada ya mafunzo hayo, washiriki watakaofaulu watakuwa na wajibu wa kwenda kufundisha wasimamizi wa makarani wa sensa ngazi ya wilaya, tarafa, shehia kwa muda wa siku 21 kuanzia tarehe 29 Julai hadi 18 Agosti 2022.

"Wito wangu kwa watendaji wenzangu katika ngazi ya mkoa, wilaya, kata, mitaa na shehia, tuhakikishe tunafuata utaratibu na kuweka uzalendo mbele na busara katika kufanikisha zoezi hili la kitaifa na kimataifa nchini," alisema Dk. Chuwa.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na wakuu wa nchi mbalimbali wa Afrika katika mkutano wa faragha wa Wakuu wa Nchi za Afrika zinazonufaika na dirisha la Maendeleo la Kimataifa (IDA 20), jijini Dakar nchini Senegal jana. **PICHA: IKULU**

# Wakuu wa mikoa watapeliwa viwanja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amebainisha namna wakuu wa mikoa ya Songwe na Mbeya walivyoliziwa viwanja vyao wanavyomiliki katika Jiji la Dodoma.

Mtaka alibainisha hayo jana jijini hapo katika kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama cha Mkoa kilichowakutanisha na watumishi wapya wa Idara ya Ardhi.

Alisema baadhi ya watumishi wa Idara ya Ardhi katika Jiji la Dodoma wametengeneza migogoro mingi kwa wananchi kwa kutoa hati ya kiwanja kimoja kwa watu wawili, kitu ambacho kimewakumba wakuu hao.

"Nimekuwa nikipokea malalamiko kuhusu hili kwa wananchi na limewakumba hata wakuu wa mikoa ya Songwe na Mbeya, wameliziwa viwanja vyao na tayari kuna watu wanajenga, hili linahitaji kushughulikiwa, tunataka migogoro ya ardhi Dodoma iishe," aliagiza.

Alisema hatawavumilia watumishi wanaosababisha migogoro ya mara kwa mara kwa kuwa wanawafanya watumishi wengine washindwe kuwahudumia wananchi na kutumia muda mwingi zaidi kutatua au kuendesha mazungumzo ya migogoro.

Mtaka aliwataka watumishi waliohamia katika jiji hilo kuwa makini na waache tamaa ya utajiri wa haraka kwa kuwa wanawatazama kwa jicho pana.

"Unakuta mtu ana shamba lake, wapimaji wanakwenda kupima kisha wanamwondoa pale wanamwambia hapa kapewa mtu mwingine na mhusika atatafutiwa sehemu nyingine, nyie nyie, hebu mwogopeni Mungu, vilio vya wananchi hawa ukivisikiliza vinakuumiza sana.

"Fikiri kama shamba hilo lingekuwa la baba au babu yako, ungemfanyia vitendo kama hivyo au ndiyo mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu?" Alihoji.

Alimtaka Kamishna Msaidizi wa Ardhi kukaa na wataalamu kuangalia namna ya kuwagawa maofisa ili kushughulikia suala la migogoro ya ardhi.

"Na wananchi waone kwamba migogoro ya ardhi imetafutiwa ufumbuzi na makosa ya nyuma yaliyofanyika ya utwaaji wa ardhi ya wananchi na kuleta manung'uniko, yasijirudie na kila mtaalamu aogope dhuluma," aliagiza.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Fatuma Mganga, alisema licha ya jiji hilo ardhi yake kupimwa, sasa linaongoza kwa kuwa na migogoro mingi.

"Jiji la Dodoma ndilo linaloongoza kwa migogoro, kwa hiyo kama mlipima lakini kulikuwa na walakini ambao umezalisha migogoro mingi sana, hiyo ndio meseji yangu.

"Kwa hiyo, nyie mliohamishiwa hapa, ni kweli jiji limepimwa lakini linaongoza kwa migogoro hapa nchini," alisema.

Alibainisha kuwa asilimia 90 ya wageni wanaofika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kwake ni wanaolalamikia haki zao za ardhi ambapo wamezunguka sana jiji bila kupata suluhisho.

Mstahiki Meya wa Jiji hilo, Prof. Davis Mwamfupe, alisema mara nyingi amepokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa wamejibiwa mafaili hayaonekani.

"Tuambieni ukweli tu mtu anapojibiwa kuwa faili lake halionekani maana yake kiwanja hicho kipo sokoni kinatafutiwa mtu mwingine auziwe na ndiyo sababu ya kiwanja kimoja kumilikiwa na watu zaidi ya mmoja.

"Mara nyingi nilipoletewa kesi ya namna hiyo nikimwita mhusika akijiumauma kwenye majibu, huwa ninamwambia aniandikie kimaandishi kuwa faili la fulani halionekani, atakwambia ngoja nikajaribu tena baadaye anakuja nalo na kusingizia kuwa lilikuwa lilichanganywa kwenye ofisi nyingine," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru, alibainisha kuwa watumishi wawili wa kitengo cha ardhi wamefukuzwa kazi na wengine watano wamesimamishwa kazi kutokana na kusababisha migogoro ya ardhi.


Mafuru alisema sababu iliyowaingiza katika matatizo watumishi hao, ni uuzaji na viwanja na kubadili matumizi ya maeneo kwa lengo la kujipatia kipato.

"Kwa mfano mzuri ni eneo lile la Mwanga Bar, tangu mwaka 1978 ni eneo wazi lakini mtu ghafla kaibuka na kubadili matumizi yake, eti akapima viwanja na watu wakaanza kujenga, hilo ni tatizo," alisema.

## ANATAFUTWA



Ndugu **Fadhili Juma Ngogota** pichani anatafutwa na polisi Kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kinyume na maadili ametafutwa muda mrefu bila mafanikio taarifa imeripotiwa polisi no. **BUG/RB/3520/2022 Tarehe 2/7/22** yeyote mwenye taarifa zake anaombwa atoe taarifa polisi kituo cha karibu nae.



IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY)
(ONE STOP JUDICIAL CENTER)
AT TEMEKE

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 48 OF 2022

In the Matter of the Estate of the Late PATRICIA FORTUNATA MWANUKUZI

AND

In the matter of Administration by MARGARET MALWA BANDORA

NOTICE TO CREDITORS

(Rule 111)

**NOTICE** is hereby given that, all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above named **PATRICIA FORTUNATA MWANUKUZI** deceased, who died at Dar es Salaam on the 13th day of May, 2020 and probate of whose letters of Administration was granted to me by the court on the 25th day of May 2022, are hereby required to send in their claims to me at the following address **"MARGARET MALWA BANDORA P.O.BOX 3457, DAR ES SALAAM"** within **60** days from the date of the publication of this notice at the expiration of which time I shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims of which I shall then have had notice.

Margaret Malwa Bandora
(Administratrix)

1|Page

# Kibano maduka nje ya hospitali chaja

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema haitahuisha vibali vya maduka ya dawa nje ya hospitali ambayo yanatakiwa kuwa umbali wa mita 500 mwaka huu wa fedha.

Januari 24, mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitangaza kuwa maduka yote ya dawa yanatakiwa kuwa umbali wa mita 500 kutoka ndani ya hospitali na kubainisha kuwa wameshatoa muda wa kutosha hadi Juni 30 mwaka huu yaondolewe.

Hata hivyo, ufuatiliaji wa Nipashe kuhusu agizo hilo katika maeneo mbalimbali, umebaini bado maduka hayo yanaendelea kutoa huduma hiyo licha ya muda wa kuwapo kwake kuisha.

Mganga Mkuu wa Serikali, Aifello Sichalwe, alipoulizwa na Nipashe kuhusiana na hilo juzi, alisema kwa mwaka huu wa fedha, hawatahuisha vibali vyao na hivyo hawatakuwa na sifa ya kuendesha biashara hiyo. "Ni kweli utaratibu wa kuyaidhinisha na kuyaondoa maduka upo kwa mujibu wa sheria, kwa sasa suala hili litajadiliwa kwenye bodi ili yafutwe, huu ni utaratibu, lazima ufuatwe," alisema.

Wakati anatoa tamko kuhusu suala hilo, Waziri Ummy alihoji sababu za hospitali kukosa dawa lakini maduka ya nje ya hospitali hizo yana dawa.

"Wamiliki wanafanya kinyume cha sheria, nipo na Mfamasia Mkuu wa Serikali, tulitunga na tulipitisha kanuni maduka yote yawe mita 500 kutoka hospitalini, nikaambiwa 'waziri kuna wengine walipewa leseni kabla', hivyo tumebakisha miezi mitano, hakuna cha msalie mtume wala kuomba radhi," aliagiza sema siku hiyo. Waziri Ummy alitangaza kuwa wanakwenda kuyaondoa ifikapo Julai Mosi mwaka huu.

# TAMISEMI yatoa hadhari wanaokula fedha mbichi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imesema katika mwaka huu wa fedha, haitavumilia wala kumwonea huruma mtendaji atakayetumia fedha mbichi kwenye halmashauri nchini.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia afya, Dk. Grace Magembe, alitoa onyo hilo jana jijini hapo alipofungua kikao kazi cha siku mbili cha makatibu tawala wasaidizi wa mikoa sehemu ya mipango na uratibu na sehemu ya usimamizi wa serikali za mitaa, maofisa mipango takwimu na ufuatiliaji na waweka hazina wa halmashauri.

Kikao hicho kina lengo la kujadili tathmini ya utekelezaji wa mipango na bajeti ya mwaka 2021/22 na uchambuzi wa mipango na bajeti ya mwaka 2022/23.

Alisema pamoja na kuwapo kwa miongozo ya usimamizi wa masuala ya fedha nchini, bado kuna kesi nyingi za matumizi ya fedha mbichi kwenye halmashauri.

"Niendelee kukemea matumizi ya fedha mbichi na niwatake kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuchukua hatua kwa wakati kwa watendaji watakaoshindwa kutimiza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma," alisema.

Alisema watendaji hao wanatakiwa kuhakikisha wanaratibu na kusimamia upelekaji benki kwa wakati fedha za makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri.

"Nyie ndiyo wasimamizi wakuu, sasa kwanini mnaruhusu fedha mbichi kutafunwa? Kwenye bajeti ya mwaka mpya wa fedha 2022/23 hatutakuwa na huruma, atakayetafuna atachukuliwa hatua," alionya.

Naibu Katibu huyo alisema kuna mashine za kukusanya zimezimwa na nyingine zimeharibika, hivyo ni wajibu wao kusimamia isitokee hali hiyo.

Alizitaka mamlaka za serikali za mitaa kuomba kibali cha kubadili matumizi ya fedha pale ambapo wanataka kufanya hivyo ili kuto-



kumbana na hoja za ukaguzi.

Aliagiza kusimamia uandaaji wa taarifa ya mwisho ya hesabu za fedha za mamlaka hizo na kuwasilisha kwa wakati kwa usahihi na kudai kuwa suala hilo litakuwa kigezo cha utendaji kazi wao.

Dk. Magembe alisema kuanzia sasa utendaji wa sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa utapimwa kwa vigezo vya upelekaji wa fedha kwenye miradi asilimia 40 kwa 60.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka ofisi hiyo, John Cheyo, alisema madhumuni ya kikao hicho ni kuangalia utekelezaji wa bajeti iliyopita na kutatua kero zilizojitokeza.

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ramadhan Kailima, alisema kutakuwapo na uwajibishaji wa wasiotimiza majukumu yao vizuri.

# RC apiga marufuku walimu kuwekwa ndani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, (Pichani) amepiga marufuku walimu kuwekwa rumande kwa makosa yoyote yasiyokuwa ya kijinai.

Shigela alitoa agizo hilo juzi wakati wa akifungua kikao cha wadau wa elimu wa mkoa wa Morogoro katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM) kilicholenga kutathmini masuala ya sekta hiyo.

Kikao kazi hicho cha wadau wa sekta ya elimu mkoa kilibeba kaulimbiu isemayo "Ushirikishwaji wa Wadau kwa Elimu Bora".

Alisema licha ya kwamba mambo hayo hayajatokea ndani ya mkoa, lakini ikitokea mwalimu amekiuka mambo fulani ambayo si ya kijinai, ni marufuku kumweka ndani.

"RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa) upo hapa. Sipendezewi na sitaki kuona walimu wanawekwa ndani. Akiwekwa ndani kesho yake unaingia darasani kufundisha. Ziko njia nyingi za kumwonya, ninataka jambo hili lisiwapo mkoani hapa na kama lilishatokea, lisijirudie tena," alionya.

Mkuu wa mkoa alisema endapo kuna mwalimu hatimizi wajibu



wake vizuri na hajafanya jambo lolote la kijinai, hakuna sababu ya kumweka ndani.

Aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote ndani ya mkoa wakishirikiana na wadhibiti ubora wa elimu kuhakikisha shule zote ambazo hazijasajiliwa na serikali kuharakisha kuziwezesha kupata sifa za kusajiliwa.

Mkuu wa mkoa alisema hatua hiyo itapunguza mrundikano wa wanafunzi katika baadhi ya shule zilizoko kwenye halmashauri.

Katika hatua nyingine, Shigela aliwataka wakuu wa shule za sekondari na walimu wakuu wa shule za msingi kuwa wabunifu katika shule zao kulingana na mazingira yao.

Shigela aliwataka wakishirikiana na viongozi wa ngazi mbalimbali za vijiji na kata katika kuziendeleza shule zao kwa kuwa jambo hilo litaleta hamasa ya kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

Naye Ofisa Elimu wa Mkoa wa Morogoro, Germana Mung'aho, alisema wanafunzi 210 wa shule za msingi na sekondari wamerudi kuendelea na masomo katika mfumo rasmi baada ya kuacha kwa sababu mbalimbali zikiwamo mimba na utoro sugu.

Mung'aho alisema kupitia wadau mbalimbali wa sekta ya elimu, mkoa umetekeleza kwa kiwango kikubwa agizo la Rais la wanafunzi waliocha shule kwa sababu mbalimbali kurudi shuleni katika mfumo rasmi.

Alisema kati ya walionufaika kurudi kuendelea na masomo wako wasichana 10 waliokuwa wamepata mimba wakiwa wanasoma shule za sekondari za halmashauri ndani ya mkoa.

Kwa upande wa shule za msingi, alisema wanafunzi 200 wamerudi shuleni na kati ya hao 98 ni wasichana waliacha kutokana na sababu nyingine na wavulana wakiwa 69.

Mung'aho alisema katika idadi hiyo pia kuna wanafunzi 12 wa kike waliokuwa watoro sugu na wavulana 21 ambao nao wamerudi kuendelea na masomo.

# 800 wajitosa kuwania uongozi CCM Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANACHAMA 813 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma wamejitosa kuwania nafasi mbalimbali, huku sita wakijitokeza kwa nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa. Miongoni mwa waliojitosa kuwania Uenyekiti wa Mkoa ni Mbunge wa Afrika Mashariki, Adam Kimbisa.

Akizungumza na Nipashe jana jijini hapa, Katibu wa CCM mkoani humo, Pili Augustino, aliwataja wengine wanaowania nafasi hiyo ni Godwin Mkanwa ambaye anataka kutetea kiti chake, Hamza Mafita, Mohamed Mgoli, Emanuel Kamala na Robert Mwinje.

Alisema kwa ngazi ya wilaya waliojitokeza kugombea Uenyekiti kwa Bahi (5), Chamwino (5), Chemba (3), Dodoma Mjini (8), Kondoa (10), Kongwa (9) na Mpwampwa (5).

"Katika nafasi hizi ngazi ya wilaya, Dodoma Mjini wanawake wapo wawili, Kondoa mmoja, mpaka sasa kwenye hizi wilaya zingine wanawake hawajajitokeza, lakini bado tunaendelea na utoaji fomu," alisema.

Alisema kati ya waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali, wanaume 603 na wanawake ni 210.

Aliwahimiza wanawake wajitokeze kuwania nafasi hizo kwa kuwa na wao wana uwezo wa kuwa viongozi wazuri kama alivyo Rais Samia Suluhu Hassan.

"Rai yangu, ninawahamasisha wanachama wa CCM na jumuiya zake kuendelea kuchukua fomu kwa kuwa zinatolewa bure na hazilipiwi fedha, wajitokeze ili kupata viongozi bora,"alisema.

Alikemea vitendo vya rushwa kwa wanaCCM wanaowania nafasi hizo ambazo uchaguzi wake utafanyika Novemba mwaka huu.

"Tusitoe rushwa itakuwa ni jambo la ajabu sana tunakwenda kugombea ndani ya chama tunatoa rushwa tutajikuta tunapata viongozi ambao siyo wazuri.

"Ni vizuri wanaCCM kujua kwamba wanapopokea rushwa, inawezekana anayetoa siyo kiongozi bora, ni mtu wa kutaka tu madaraka kwa maslahi yake na siyo kuwatumikia wanaCCM, sisi CCM tuwe mfano bora kwa wananchi," alisema.


Date: 30th June, 2022.

IN THE MATTER OF MSOKE NASHALO FARMS LIMITED
AND
IN THE MATTER OF THE COMPANIES ACT No. 12 OF 2002
NOTICE TO CONTRIBUTORIES/THE THEN SHAREHOLDERS OF MSOKE NASHALO FARMS LIMITED

**NOTICE** It is hereby given to the contributories/the then shareholders of **Msoke Nashalo Farms Limited** that by an Order of the High Court **(Hon. Mutungi, J)** dated 13th June, 2022, in the High Court of Tanzania (Moshi District Registry) in Petition No. 4 of 2021 ordered that the affairs of **MSOKE NASHALO FARMS LIMITED** (the "Company") be wound up by the Court in accordance with the provisions of the Companies Act, 2002

**FURTHER NOTICE** is given that:

1. We, **Hellen Mahuna** of P. O. Box 1462 NSSF Kilimanjaro Commercial Complex, 2nd Floor Room No. 5 Moshi and **Jerimiah Tarimo** of P. O. Box 15159 Dar es Salaam were appointed Liquidators by the High Court for purposes of winding up the above cited Company,
2. ALL contributories of the Company are hereby given legal notice to appear on the contributories meeting fixed by the appointed liquidators on 29th July, 2022 at **Panama Hotel Shanty Town Moshi at 10:00 am** in order to ascertain their wishes in all matters concerning liquidation.
3. Take further note that every contributory/the then shareholder have to appear in person, or any person thereof representing contributory must appear with a written proxy to that effect. Note that all proxies shall reach the office of the liquidators located at NSSF Kilimanjaro Commercial Complex, 2nd Floor Room No. 5 Moshi on or before 25th July 2022 at 0400pm

SIGNED at Moshi this 30th day of June, 2022

**Hellen Mahuna**
For and on Behalf of Liquidators.

216935402



**THE COMPANIES ACT, CAP 212 (R.E 2002)**
**TRANSSNET PAYMENT TANZANIA LIMITED**

**NOTICE OF RESOLUTION TO WIND UP VOLUNTARILY BY MEMBERS**

**NOTICE** is hereby given to the general public that by special resolution dated **23rd May 2022, TRANSSNET PAYMENT TANZANIA LIMITED** resolved to wind up the company voluntarily by members.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT, WINSTLAW ATTORNEYS, of P.O BOX 32080** Dar es salaam was appointed as liquidator for the purpose of winding up **TRANSSNET PAYMENT TANZANIA LIMITED.**

**TAKE NOTICE** that all the creditors are hereby requested to furnish the liquidator with full details of their claims against the company at the address below within fourteen days (14 days) from the date this notice has been published.

**Dated and signed this 1st June 2022**

Winstlaw Attorneys, Liquidator
Edrick Luimuka, Advocate

**ADDRESS:**
**WINSTLAW ATTORNEYS**
**ALI HASSANI MWINYI ROAD, CHABRUMA STREET**
**JANGID PLAZA, 03RD FLOOR,**
**P.O BOX 32080**
**DAR ES SALAAM**

216934002



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na mkewe Mama Mariam Mwinyi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, wakimsikiliza Mwakilishi wa kikundi kutoka Burundi, Chantal Birarondekwa (kulia), wakati walipotembelea maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali, katika maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali yaanika mikakati ya kueneza Kiswahili kimataifa

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali imejipanga vyema kueneza lugha ya Kiswahili duniani na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kuifanya lugha hiyo ijuze kimataifa.

Alibainisha hayo jana kupitia ujumbe wake kwa njia ya video wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili iliyokwenda sambamba na kutambua mchango wa lugha hiyo katika ukombozi wa Bara la Afrika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

"Uzinduzi huu wa leo (jana) utaongeza kazi, miundombinu na bajeti kwa mabaraza, taasisi na vyuo vinavyofundisha Kiswahili ili viendelee kuandaa wataalamu zaidi watakaotumika duniani kote," alisema.

Rais Samia aliitaja baadhi ya mikakati iliyopo kuwa ni kuziwezesha ofisi za kibalozi zilizopo nje ya Tanzania kuhamasisha uanzishwaji wa vituo vya kufundisha lugha hiyo kwa wageni ambapo walimu wake watakuwa ni vijana waliohitimu katika vyuo vikuu.

Alisema pia watawapatia nyenzo na kuwajengea uwezo wa taaluma ya tafsiri, uhariri, ufundishaji wa lugha kwa wageni, utangazaji na uandishi wa Kiswahili kwa wanaojihusisha na taaluma hizo.

Rais alilishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kuitenga siku hiyo kuwa ya Kiswahili duniani kwa kuwa imeipa lugha hiyo heshima na hadhi kubwa.

MAAGIZO YA SERIKALI

Katika kutekeleza mpango wa kukuza lugha hiyo, Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, aliyekuwa mgeni rasmi, alitoa maagizo mbalimbali ikiwamo kwa wizara na taasisi za serikali.

Alizitaka wizara na taasisi hizo kutekeleza maagizo ya serikali ya nyaraka za mawasiliano za wizara na idara zake, mikutano, warsha, semina na mijadala ya umma na dhifa ziwe kwa lugha ya Kiswahili.

Makamu wa Rais pia aliagiza majina ya mitaa, barabara, mabango, fomu za usaili na maelekezo ya matumizi ya dawa zote na bidhaa na huduma pia ziandikwe kwa lugha hiyo. Huku taarifa za miradi na mikataba inayohusu wananchi ziwe kwa lugha ya Kiswahili.

"Jambo la tatu, sheria na kanuni ambazo bado hazijatafsiriwa, zitafsiriwe na wizara na taasisi zinazosimamia sheria na kanuni hizo kwa kushirikiana na mabaraza ya Kiswahili, wataalamu wengine wa Kiswahili na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali," aliagiza.

Vilevile, aliviagiza vyombo vya habari vinavyotumia lugha hiyo, kuitumia kwa ufasaha huku vikizingatia sarufi ya Kiswahili na kutoa tafsiri ya maneno yasiyo ya Kiswahili.

Makamu wa Rais alisema katika miaka ya karibuni, kumekuwa na ongezeko la upotoshaji wa matumizi ya lugha hiyo miongoni mwa jamii hususan vijana na kutoa rai kwa wataalamu na watumiaji wa lugha hiyo kuendelea kuongea Kiswahili fasaha na kuandika vitabu vya taaluma mbalimbali vya lugha hiyo.

"Kwa hali ilivyo sasa, ni dhahiri kuwa tuna uhitaji mkubwa wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia lugha ya Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, hatuna budi kukidhi haja hii.

"Ninawapongeza wale wote wanaotumia mitandao ya kijamii na TEHAMA kwa ujumla kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili," alisema.

**MAKUBALIANO 'SAUZI'**

Katika hafla hiyo, Makamu wa Rais alishuhudia utiaji saini wa makubaliano kati ya Wizara ya Elimu ya Tanzania na Afrika Kusini ya ushirikiano katika elimu ya msingi ikiwamo kuipatia nchi hiyo nyenzo na wataalamu wa kufundisha Kiswahili kwa shule za msingi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema kuwa ikiwa kama nchi mwasisi na vinara wa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha, Tanzania ina wajibu wa kuikuza na kuiendeleza lugha hiyo.

"Tumekubaliana na waziri mwenzangu baada ya kutia saini makubaliano haya, sasa tutaanza kuandaa mpango kazi na tutaalika timu za ufundi kutoka Afrika ya Kusini zije hapa zikutane na timu zetu zinazoongozwa na katibu mkuu wetu (Dk. Francis Michael) kwa ajili ya kujadiliana namna ya kutekeleza makubaliano haya," alisema Mkenda.

Waziri wa Elimu wa Afrika Kusini, Angelina Motshekga, alisema lengo la nchi hiyo ni kukifundisha Kiswahili katika ngazi zote za elimu na kuwa baada ya kutangaza nia ya kufundisha lugha hiyo, Tanzania ndiyo ilikuwa ya kwanza kuomba kutoa nyenzo za ufundishaji na walimu.

Aliongeza kuwa nchi hiyo inathamini Kiswahili kama lugha itakayowaunganisha na kuwaweka karibu na nchi zingine za Kiafrika ukizingatia kuwa bara hilo linahitaji kushikamana kutokana na ubaguzi wa rangi.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, alisema maadhimisho hayo yaliyofanyika kwa siku saba ni maagizo ya UNESCO yaliyoitaka dunia kuadhimisha mchango wa lugha hiyo kila Julai 7.

Mwakilishi Mkazi wa UNESCO nchini alisema shirika hilo linathamini matumizi ya lugha mbalimbali ikiwamo Kiswahili na kuwa kukua kwa lugha hiyo kunatoa historia ya karne za mabadiliko ya dunia.

"Kiswahili ni miongozi mwa lugha 10 zinazozungumzwa sana duniani na kujenga utengamano miongoni mwa jamii na mataifa mbalimbali. Ni lugha ya kurusha habari lakini pia ni lugha ya elimu." alisema.

Akitoa salamu za pongezi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Filipe Nyusi, alisema ni tunu na heshima kubwa kwa wazungumzaji wote wa Kiswahili duniani kuadhimisha siku hiyo kwa kuwa lugha hiyo ina umuhimu mkubwa katika kurahisisha mawasiliano na kuunganisha watu wa mataifa mbalimbali.

"Kiswahili ni kielelezo cha pekee cha desturi na utamaduni wetu, ustaarabu pamoja na fikra zetu. Kiswahili kinarahisisha na kutuwezesha kupata habari, mawazo mapya, elimu na maarifa, pia kumiliki sayansi na teknolojia," alisema Rais huyo.

# Dk. Mwinyi aona fursa ajira lugha ya Kiswahili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema lugha ya Kiswahili ni moja ya fursa ya kupata ajira, hivyo vijana wanapaswa kuitumia vizuri.

Amesema matumizi ya lugha hiyo sasa yameongezeka na kupenya haraka katika Afrika ya Mashariki, Bara la Afrika na ulimwenguni kote baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuipa hadhi lugha hiyo kimataifa.

Akizungumza jana katika maadhimisho ya Siku ya Kiswahili kwenye Hoteli ya Golden Tulip mjini Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema Kiswahili ni daraja la kuwaunganisha wananchi, hivyo ni vyema kuzitumia fursa zinazopatikana zikiwamo za kibiashara na kiuchumi.

Dk. Mwinyi alisema viongozi wa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) walichukuwa uamuzi sahihi wa kuitangaza lugha ya Kiswahili ili kutumiwa na wananchi wa nchi hizo kuongeza utengamano utakaowaunganisha wananchi wake katika shughuli zote muhimu za maendeleo.

Alisema mafanikio ya Kiswahili kutoka Afrika na kuenea katika mabara mengine ni dalili njema ya kutambua umuhimu wa Kiswahili katika maendeleo ya mataifa yao.

"Lugha ya Kiswahili ni fursa, hivyo vijana wanapaswa kutambua kuwa Kiswahili ni bidhaa inayouzika na kuwapatia ajira," alisema.

Dk. Mwinyi alisema mkutano wa kikao cha 21 cha viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Februari 2021, uliidhinisha Kiswahili kama lugha rasmi ya jumuiya hiyo na sasa ni lugha ya kazi katika mikutano ya kimataifa ikiwamo Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU).

"Tuna wajibu sisi wenyewe kuonyesha mapenzi ya lugha yetu hii kwa kuizungumza kwa ufasaha na usahihi ili kuwa walimu wazuri kwa wale wanaojifunza," aliagiza.

Alisema taasisi zinazosimamia maendeleo ya Kiswahili, zina wajibu wa kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kuiendeleza lugha hiyo ikiwamo kutoa mafunzo na kufanya utafiti wa isimu na fasihi na kusaidia watunzi wa vitabu na machapisho yatakayosaidia kukuza Kiswahili.

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki waTanzania, Balozi Joseph Sokoine, alisema wakati umefika kwa nchi wanachama kuhakikisha Kiswahili kinatumika kikamilifu kwa ajili ya kuunganisha nchi wanachama katika shughuli zao muhimu, zikiwamo za kisiasa, kiuchumi na kibiashara.

Alisema Kiswahili ni lugha maarufu Tanzania, ikitumika katika shughuli muhimu za kudai uhuru kutoka kwa wakoloni na hata katika vyombo muhimu vya kutunga sheria.

"Wakati umefika kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kukitumia Kiswahili kikamilifu kwa ajili ya kuwaunganisha wananchi wake ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa azimio la viongozi wa nchi wa jumuiya hiyo," alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), Steven Mlote, alizipongeza nchi wanachama wa jumuiya hiyo kwa ushirikiano wao ambao umetoa nafasi kubwa katika ukuaji wa Kiswahili kupitia Kamisheni ya Kiswahili (KAKAMA).

Alisema amefurahishwa na uamuzi wa baadhi ya nchi wanachama ikiwamo Sudan Kusini kutumia lugha hiyo katika ngazi ya kufundishwa shuleni.

Washiriki wa maadhimisho ya siku hiyo kutoka nchi jirani ikiwamo Uganda, Rwanda, Kenya na Burundi walisema watahakikisha Kiswahili kinatumika nchini mwao katika kufundishia kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi vyuo vikuu.

HABARI KITAIFA

# Halmashauri Rombo hatarini kupokwa mil. 700/- upangaji, umilikishaji ardhi

**Na Munir Shemweta**, ROMBO

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameipa mwezi mmoja Halmashauri ya Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro kutekeleza mradi wa kupima, kupanga na kumilikisha ardhi ifikapo Julai 31, mwaka huu.

Amesema kinyume cha hapo Sh. milioni 700 kati ya bilioni 1.06 ilizopewa kwa ajili ya mradi huo, zitahamishiwa halmashauri zingine za mkoa huo.

Hatua ya Dk. Mabula inatokana na halmashauri hiyo kushindwa kutekeleza mradi huo kwa wakati na hadi sasa imetumia Sh. milioni 60 tu.

Kwa mujibu wa waziri, halmashauri hiyo inaonyesha kama haistahili kupata fedha za mradi huo pamoja na kuwa na andiko zuri la kupatiwa fedha kwa ajili ya utekekezaji wa mradi huo.

Rombo iliomba Sh. bilioni 1.06 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika eneo la Holili hususan kitongoji cha Holili Shuleni. Uchaguzi wa eneo hilo ulizingatia eneo lisilokuwa na maendelezo mengi kuepuka ukuaji holela wa mji.

Taarifa ilieleza kuwa halmashauri hiyo ilipanga kutwaa ardhi kupanga na kupima viwanja 400 vya ukubwa tofauti kwa ajili ya matumizi mbalimbali ambayo ni viwanja 300 kwa matumizi ya makazi, 50 kwa ajili ya makazi na biashara na 50 vya biashara.

Aidha, halmashauri hiyo imetarajia kuuza viwanja 400 na kupata Sh. bilioni 1.440 na kubakiwa na Sh. milioni 380 kama mapato ya ndani.

"Andiko na kazi mlizofanya bado haionyeshi kama kulikuwa na hitaji la halmashauri kupatiwa pesa hizo. Sheria ziko wazi kama lipo hitaji la kutwaa eneo kwa ajili ya manufaa ya umma.

"Habari ya ku- 'debate' (kujadiliana) na watu kwa muda mrefu na kukaa kimya halafu taarifa zisifike kwa wakati. Leo miezi sita mmetumia Sh. milioni 60 kati ya bilioni 1.060 tu hakuna sababu. Kama mnahitaji pesa pengine pesa mliyopewa ni nyingi kuliko mahitaji," alisema Dk. Mabula.

Akizungumza na uongozi wa Wilaya ya Rombo juzi, wilayani hapo Waziri Mabula alisema halmashauri hiyo haijalipa fidia wala kutekeleza mradi kwa kasi inayotakiwa, hivyo wizara inafikiria mara mbili uamuzi wa kuiachia halmashauri pesa yote iliyoomba kwa kuwa hitaji kwa ajili ya miradi kama hiyo liko maeneo mengi.

Kwa mujibu wa waziri, kusuasua kwa utekelezaji miradi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi nchini kwa baadhi ya halmashauri, unasababishwa na maeneo mengi wakurugenzi kutotoa ushirikiano wa dhati katika sekta ya ardhi hasa ikizingatiwa kuwa wao ni mamlaka za upangaji katika maeneo yao.




Mweka hazina wa umoja wa wazaliwa wa kijiji cha Suguti, Musoma Vijijini mkoani Mara, waishio mikoa mbalimbali nchini uitwao Suguti Diaspora, Belias Bunini, akisoma taarifa ya mapato na matumizi katika mkutano wa kawaida wa umoja huo, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakatisha masomo kisa ujauzito

**Na Julieth Mkireri**, KIBITI

WANAFUNZI wa kike 32 katika Wilaya ya Kibiti wameshindwa kuendelea na masomo yao baada ya kupata ujauzito katika kipindi cha Januari hadi Juni, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti, Mohamed Mavula, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mikakati wanayoifanya kudhibiti ongezeko la mimba kwa wanafunzi.

Mavula alisema katika kipindi cha mwaka 2020, wanafunzi waliokatisha masomo kwa kupata mimba walikuwa 22 wakati kwa mwaka 2021 walikuwa 36.

Alisema ongezeko hilo la mimba linatokana na baadhi ya wazazi kuwaacha watoto wao wajilee wakati wao wakiwa katika shughuli za kilimo mbali na makazi yao. "Asilimia 98 ya wakazi wa Kibiti ni wakulima na shughuli zao wanazifanyia katika maeneo ya delta na Rufiji hivyo wakati wa kilimo wanaenda huko na kuwaacha watoto peke yao," alisema Mavula.

Kutokana na hali hiyo, Mavula alielezea mikakati waliyo nayo kuwa ni pamoja na kushirikiana na kamati za vijiji na waratibu wa elimu kuendelea kutoa elimu kwa wazazi kuithamini elimu pamoja na kupanga namna ya watoto wao watakavyoishi wakiwa kwenye shughuli za kilimo.

Mmoja wa wakazi wa kijiji cha Kinyanya, Kata ya Mtawanya, Hamis Abdallah, alisema suala la ongezeko la mimba kwa watoto wa wilaya ya Kibiti ni pamoja na wazazi kuwa na usimamizi mdogo kwa watoto wao.

Hamis pia alisema hali duni kwa baadhi ya wazazi inachangia kuwaingiza watoto wao kwenye vishawishi wanaporubuniwa kupatiwa fedha za kutumia shuleni hivyo ni vema serikali ikasaidia upatikanaji wa chakula shuleni.

"Baadhi ya wazazi hali zao ni duni, watoro wanaenda shule bila hela, na wapo wengine wanasoma mbali hivyo wanashindwa kuvumilia kushinda bila kula wakikutana na mtu anampa fedha lazima washawishike, serikali iangalie uwezekano wa kuwa na chakula shuleni.

Kwa mujibu wa Diwani wa Mtawanya, Malela Toka, katika kipindi cha miezi sita mwaka huu, wanafunzi 11 katika kata yake wameripotiwa kukatisha masomo baada ya kupata mimba.

# Bil. 8.8/- zafadhili miradi sekta elimu

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA), imetumia Sh. bilioni 8.8 katika mwaka wa fedha wa 2021/22 kufadhili ujenzi wa miradi mbalimbali ya elimu nchini.

Miradi hiyo iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu na ununuzi wa vifaa vya kujifunza na kufundishia.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, wakati akimweleza Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, namna TEA ilivyofadhili ujenzi wa miundombinu kwenye shule za Iwambi na Iganjo jijini Mbeya.

Alisema TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa imetumia Sh. milioni 200 kwa ajili ya kukarabati miundombinu kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 ikiwa ni sehemu ya jitihada za serikali katika kuboresha upatikanaji wa elimu bora nchini.

Geuzye alisema kupitia mfuko huo, Shule ya Msingi Iganjo imepata ufadhili wa Sh. milioni 100 ambazo zimegharimia ujenzi wa madarasa matatu, ofisi moja ya walimu na matundu 28 ya vyoo.

Alisema katika Shule ya Msingi Iwambi mfuko umetoa ufadhili wa Sh. milioni 100 zilizotumika kujenga madarasa matatu, ofisi moja ya walimu na matundu 24 ya vyoo.

Wanafunzi 4,000 wanaosoma katika shule hizo mbili wamenufaika na ufadhili huo na alihimiza utunzaji wa miundombinu hiyo ili iweze kuwanufaisha watoto wengi wa kitanzania.

Alisema TEA ni taasisi ya umma inayofanya kazi chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Alisema TEA inaratibu Mfuko wa Elimu Taifa, ambao unaongeza jitihada za serikali katika kuboresha miundombinu ya elimu nchini kwa lengo la kuongeza ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa.

Akizungumza katika ziara hiyo, Spika wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini ambako miradi hiyo imetekelezwa, aliishukuru serikali kwa kuendelea kutenga fedha za Mfuko wa Elimu wa Taifa ambazo zinatumika kuboresha miundombinu ya elimu katika sehemu mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Mbeya.

Alisema ofisi ya Mbunge wa Mbeya Mjini itaendelea kuweka kipaumbele kwenye ujenzi wa miundombinu ya elimu ili kuongeza hali ya ufaulu kwa wanafunzi wa mkoa huo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tanzania ichangamkie fursa lugha ya Kiswahili kiuchumi

**TANZANIA** jana iliadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani ambayo pamoja na mambo mengine yamewekwa maagizo kadhaa na serikali juu ya kukuza lugha hiyo ambayo kwa sasa inasambaa kwa kasi duniani.

Kabla ya kuadhimishwa kwa siku hiyo, kulikuwa na makongamano na midahalo yenye mada mbalimbali katika kuangazia mchango wa Kiswahili katika masuala mbalimbali yakiwamo maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kusaidia mataifa mbalimbali katika harakati za kujikomboa kutoka mikononi mwa wakoloni.

Juzi, kwa mfano, kulikuwa na mdahalo jijini Dar es Salaam kuhusu mchango wa Kiswahili katika ukombozi wa Afrika. Katika mdahalo huo, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, aliliweka bayana kwamba lugha hiyo bado haijaleta matokeo chanya katika maendeleo ya kiuchumi.

Mwanasiasa huyo mkongwe alibainisha kwamba Tanzania ni mwasisi wa Kiswahili na ndiyo inayotumia lugha hiyo kwa kiwango cha juu, lakini cha ajabu haipati fursa za kutosha zinazotokana nayo yakiwamo mapato ya lugha yenyewe. Alisema mapato yanayotokana na Kiswahili duniani ni wastani wa Sh. bilioni 1.3 kwa mwaka lakini Tanzania inaambulia kiasi kidogo.

Sambamba na mapato, fursa zinazotokana na Kiswahili zikiwamo ajira kama vile kufundisha taasisi za elimu ya juu vikiwamo vyuo vikuu zinachangamkiwa na kutumiwa na mataifa mengine yakiwamo jirani kama vile Kenya.

Pia katika idhaa za Kiswahili katika vyombo vya habari vya kimataifa kwa kiasi kikubwa ni Watanzania wachache wanaopata nafasi katika vyombo hivyo. Nafasi zingine ni za wakalimani wengi katika vyombo na taasisi za kimataifa wanatoka kwenye mataifa mengine nje ya Tanzania.

Sambamba na Kinana, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kiswahili visiwani humo, aliwataka vijana kutokulala badala yake wachangamkie fursa zinazotokana na Kiswahili badala ya kuachia watu kutoka mataifa mengine.

Ni wazi kwamba kilichosemwa na viongozi hao pamoja na watu wengine walioshiriki kutoa mada au michango katika maadhimisho hayo ni mambo ya msingi. Kuna fursa nyingi za kiuchumi na kijamii zikiwamo ajira kwenye mashirika ya kimataifa lakini ni Watazania wachache wanaothubutu.


Kauli ya Kinana na Rais Dk. Mwinyi zinapaswa kuwa mwangwi wa kuwaamsha Watanzania katika kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza ikiwamo inayotokana na lugha ya Kiswahili.

Jambo la kujiuliza ni kwamba kutokana na Kiswahili kutumika katika mataifa mbalimbali ikiwamo Umoja wa Afrika (AU), ni Watanzania wangapi wamejitokeza kuchangamkia kazi zinazotangazwa zikiwamo za ukalimani? Hata katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Bunge lake (EALA) ambako makao makuu yako nchini Tanzania mkoani Arusha, ni Watanzania wangapi wanafanya kazi zinazohusiana na Kiswahili?

Hivi sasa mataifa mbalimbali yamefungua milango katika taasisi zao kuanza kufundisha Kiswahili, hivyo ni wakati mwafaka kwa Watanzania wakiwamo walimu kuchangamkia fursa hizo kwa ajili ya kujipatia ajira.

Ni dhahiri kwamba kama vijana wataanza kuchangamkia nafasi za ajira husussan katika taasisi za kimataifa zinazofundisha au kutumia Kiswahili, tatizo la ajira ambalo limekuwa wimbo usio na mwisho, litapungua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Fanya hivi ili usitapeliwe ardhi yako inauzwa kwa watu wawili

Na Halfani Chusi

**UKINUNUA** ardhi kwa maana ya nyumba, kiwanja, au shamba hakikisha unafanya uhamisho wa miliki kutoka kwa aliyekuuzia na kusomeka kwa jina lako mara moja kadri iwezekanavyo, ili kujiepusha na mambo mengi, ikiwamo kutapeliwa au kuuziwa kiwanja kimoja mara mbili.

Wengi tukinunua viwanja kwa sababu hakuna anayetuuliza wala kutulazimisha kufanya uhamisho kwa haraka basi tukishakabidhiwa hati na mikataba ya mauziano tunakaa nazo hata miaka miwili au mitatu, huku tukisema nikipata pesa nitaenda kubadilisha umiliki hilo ni kosa kubwa.

Inapaswa kutambua kuwa, kama haujabadilisha jina kutoka kwa mmiliki wa ardhi aliyekuuzia, kuna uwezekano mkubwa aliyekuuzia akakuzunguka na kukiuza kwa mtu mwingine na hata kukuchezea anakuwa na uwezo mkubwa.

Nilipopiga stori na Wakili wa Kujitegemea, Bashiru Yakubu, alinieleza mengi ikiwamo namna watu wanavyodhulumika na kukosa haki kwa kutokujua umuhimu wa kufanyia uhamisho.

Akanidokeza kwa darasa: "Mfano ni kwamba, kuwa aliyekuuzia anaweza kutoa taarifa ya kupotelewa kwa hati kituo cha polisi kisha akapewa kibali kinachoonyesha kupotea kwa hati (loss report) anaendelea

"Baada ya hapo akafanya tangazo kwenye radio, tv, na kwenye magazeti ya serikali na binafsi halafu akafanya maombi ya kupatiwa hati mpya kupitia Fomu namna Tatu chini ya Kifungu cha 38 cha Serikali ya Usajili wa Ardhi Sura ya 334."

Kisha hapo mtu anapatiwa hati nyingine mpya, hiyo inafanya kutakuwapo hati mbili katika ardhi moja. Huo tayari unakuwa kiashiria cha mgogoro, kwako mnunuzi usiye na hati.

Akishakuwa na hati, hayo mengine anaweza kuyakataa kirahisi na pengine watu wa namna hii hata zile saini anazokuwa amekuwekea kwenye nyaraka nyingine, zinaweza kuwa sio zake.

**"Baada ya hapo akafanya tangazo kwenye radio, tv, na kwenye magazeti ya serikali na binafsi halafu akafanya maombi ya kupatiwa hati mpya kupitia Fomu namna Tatu chini ya Kifungu cha 38 cha Serikali ya Usajili wa Ardhi Sura ya 334."**

Mbaya zaidi, ni kwamba mtu usipofanya uhamisho na wakati umeshanunua shughuli zote zinazohusu ardhi hiyo mfano kulipa kodi za ardhi, vibali vya ujenzi, tathmini, tozo na kila kitu kinaendelea kusoma jina la aliyekuuzia na malipo yataendelea fanyika kwa jina la aliyekuuzia.

Maana yake ni kwamba, ushahidi wote wa risiti na nyaraka nyinginezo unaendelea kumtambua aliyekuuzia kuwa mmiliki halali wa ardhi hiyo ambapo anaweza kutumia ushahidi huo dhidi yako na ukakosa haki.

Hiyo ni kwa sababu, ataonyesha risiti znazosoma jina lake na atasema nilikuwa nalipia atachukua hata kibali cha ujenzi bila wewe kujua na atakioonyesha kinasoma yeye.

Ndugu yangu, katika mazingira hayo kushinda kesi hiyo kunahitaji muujiza wa Mwenyezi Mungu, kama utabahatika kuzipata, lakini kama umefanya uhamisho mchezo huo ni mgumu sana na pengine haitawezekana kabisa.

Nasema, hata ikiwezekana kwa nguvu ya rushwa au utumiaji wa mamlaka, bado mnunuzi utakuwa salama kwa sababu ya mfumo utaonyesha umiliki ulivyokuwa ukihamishwa kutoka kwa mmiliki mmoja kwenda kwa mwingine.

Ninachotaka kushauri, unaponunua kiwanja au ardhi kwa lengo fulani inatakiwa kufanya uhamisho wa umiliki mapema najua wengi wetu tunaogopa gharama ambayo ni asilimia 10, lakini hiyo huwa inazungumzika na kupungua.

Pia, wakati wa kununua ardhi hakikisheni mikataba yenu inashuhudiwa na wanasheria (mawakili) wakili kwa cheo chake ni ofisa wa viapo na mthibitishaji wa umma, pia ni ofisa wa mahakama.

Wakili akiwa kwenye makataba wako wa manunuzi, ni mtu muhimu sana na ushahidi wa hakimu unaaminiwa sana na mahakma.

Waswahili wnasema heri nusu shari kuliko shari kamili katika andiko. Hili ni bora utekeleze ushauri huo ukawa salama katika ardhi yako, kuliko kupuuzia ukaingia hasara ya eneo lako kabisa na ukalikosa mjini wajanja wajanja ni wengi sana.

# Muuguzi aliyeomba rushwa asimamishwa kazi, akutwa na gongo

**Na Oscar Assenga,** LUSHOTO

MKUU wa Wilaya ya Lushoto, Kalist Lazaro, amesema kuwa Muuguzi wa Zahanati ya Kijiji cha Buheloi, John Chuma, aliyekataa kumpa huduma wakati wa kujifungua mama mjamzito, Jenifa Godson mkazi wa kijiji cha Gare wilayani Lushoto, baada ya kukosa elfu 40,000 alizoomba kama rushwa, alikutwa na pombe haramu ya gongo eneo la kazi.

Aidha, Baraza la Wauguzi na Tiba (TNMC) limemnyang'anya leseni na kumsimamisha kazi, huku polisi wakimchukulia hatua kwa kukutwa na pombe hiyo haramu.

Aidha, Mkuu huyo wa wilaya alitoa wito kwa watumishi wa kada ya afya kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa tija kuweza kuwahudumia wananchi kama walivyoomba.

"Tukio hili ni la aibu kituo chenyewe kilichotokea hakukuwa na upungufu wa vifaa tiba, wala vifaa vya kujifungulia wala dawa kilichotokea ni mapungufu ya muuguzi mwenyewe alikuwa amelewa na kutaka fedha kwa mzazi Sh. 40,000 na baadaye ikapatikana 30,000 akakataa na alipewa 40,000 akaenda kwenye nyumba ya gongo na kumuacha mama mjamzito ndani,"alisema.

Alisema alivyorudi alimsaidia kujifungua, lakini akakataa kifunga kitovu cha mtoto na kukataa kummalizia mtoto na kutoa kondo la nyuma la uzazi na kurudi kwenye gongo," alisema DC huyo.

Alisema alipopewa taarifa kwa bahati mbaya kulikuwa na nesi kwenye kituo hicho, lakini alimfungia ndani nesi jambo ambalo ni baya zaidi, na kwamba ndugu walimsaidia akapelekwa hospitali ya juu zaidi.

"Lakini matukio yake ni ya kujirudia mara kwa mara amekuwa akigonga watu na hivyo ana kesi kama hiyo ni mtu wa matukio nasema sisi tumechelewa kumjua pengeni tumechelewa kuchukua hatua," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Ikupa Mwasyoge alisema wameridhika na hatua alizochukuliwa ikiwamo kufunguliwa kesi ya kukutwa na pombe haramu ya gongo.

# TIC yawapa njia wafanyabiashara wa India

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimewaita wawekezaji kutoka nchi mbalimbali duniani kuwekeza Tanzania, huku kikiwapa utaratibu wafanyabiashara 27 kutoka India walioonyesha nia katika maeneo matano yakiwamo ujenzi wa hospitali na usindikaji.

Maeneo mengine ambayo wafanyabiashara hao wameonyesha nia ya kuwekeza ni bandari, uzalishaji wa vifungashio vya bidhaa na viwanda vya kuzalisha bidhaa zitakazouzwa nchini.

Katika hafla iliyokutanisha wafanyabiashara hao na wadau mbalimbali wa biashara iliyofanyika katika ubalozi wa India nchini jana, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, John Mnali, alisema wamewaelekeza utaratibu kulingana na aina ya uwekezaji wanaotaka kuufanya.

Wafanyabiashara hao wako nchini kushiriki Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa maarufu kama Sabasaba na kutafuta fursa ya biashara na uwekezaji Tanzania.

Alisema hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan alizindua filamu ya The Royal Tour na kushiriki makongamano kadhaa ambayo amewahakikishia wawekezaji kwamba Tanzania kuna fursa za uwekezaji na biashara.

"Mwitikio wake tunaona makundi ya wafanyabiashara wanakuja kutafuta fursa za biashara na uwekezaji, kupitia mkutano huu tumewajulisha wafanyabiashara wa India fursa mbalimbali kwa wale wanaotaka kuwekeza kwenye kilimo, madini, uvuvi na mazao ya uvuvi," alisema.

Pia alisema wamewajulisha vivutio vya kitalii wanavyovitoa kwa wawekezaji wanaowekeza maeneo mbalimbali zikiwamo taratibu kulingana na aina ya uwekezaji mtu anaoufanya.

Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan, alisema kampuni 27 kutoka India yenye kuzalisha bidhaa mbalimbali wamekuja Tanzania kwa ajili ya kuangalia fursa za biashara na uwekezaji na kutangaza bidhaa zao ili kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizo.

Alitaja baadhi ya kampuni zilizokuja ni zile zinazohusika na bidhaa za kilimo, ulinzi na usalama, plastiki, wanaozalisha vifaa vya hospitali na mashine za viwandani.

Aliushukuru ujumbe wa wafanyabiashara kutoka India uliofika nchini kupitia Shirikisho la Wauzaji wa Bidhaa za India Zinazouzwa Nje (FIEO).

"Hali ya biashara kati ya Tanzania na India ni nzuri ambapo kwa mwaka 2021, wafanyabiashara kutoka India waliuza bidhaa Tanzania zenye thamani ya Dola bilioni 2.3 (import) na Tanzania iliuza bidhaa zake nchini India zenye thamani ya dola bilioni 2.2," alisema.

Kwa upande wa uwekezaji Tanzania, alisema wafanyabiashara hao wameonyesha nia ya kuwekeza katika maeneo hayo matano.

Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Biashara kati ya India na Tanzania (TIBF), Gopal Krishnan, alisema kulingana na takwimu za TIC, zaidi ya kampuni 613 kutoka India zipo Tanzania na zimewekeza mtaji wa zaidi ya Dola bilioni 3.65 na kutoa ajira kwa Watanzania 48,184.

Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni na Majina ya Biashara kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Meinrad Rweyemamu, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanawahudumia wawekezaji kutoka nje kupitia mtandao.

"Ukitoa huduma kimtandao maana naye ndani ya muda mfupi wanazipata, tunawakaribisha waje kuwekeza na tunawaambia popote walipo wanaweza kupata huduma zetu mtandaoni.

"Lengo upate huduma kwa wakati bila usumbufu wowote, kama kila kitu umeshakifanya basi tunasajili kampuni ndani ya siku tatu na unaweza kwenda mbele kwa akili ya kupata leseni," alisema.




Mkuu wa Kitengo cha Bima cha Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Francis Kaaya (mwenye suti nyeusi), akifafanua jambo kwa wananchi, walipotembelea banda la benki hiyo, katika maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Machampioni' ukatili wazawadiwa baiskeli

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KITUO cha pamoja cha huduma ya Mkono kwa Mkono kwa watoto waliofanyiwa ukatili kilicho chini ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan mjini hapo, kimetoa baiskeli kwa machampioni 188, zenye thamani ya Sh. milioni 38.5, ili kuendelea kudhibiti vitendo hivyo.

Baiskeli hizo zilizokabidhiwa kwa machampioni hao wa mitaa ya kata 15 za manispaa hiyo, zilimetolewa na Mashirika ya Kimisionari la Miserior kutoka Ujerumani na Misean Cara wa Ireland.

Kabla ya kukabidhiwa baiskeli hizo walipatiwa mafunzo maalumu chini ya kituo cha pamoja cha huduma ya mkono kwa mkono kwa watoto, kinachosimamiwa na chuo kikuu hicho.

Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, Prof. Betram Mapunda, alisema hayo kabla ya kumkaribisha Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Morogoro, Hilary Sagara, kukikabidhi baiskeli hizo.

Alisema chuo kikuu hicho kilianzisha kituo hicho baada ya kufanya utafiti kwenye mitaa iliyopo kata mbalimbali za manispaa hiyo na kubaini kuwepo kwa changamoto ya vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watoto na wazazi, walezi na jamii inayowazunguka.

"Tulifanya utafiti wa kina katika kata mbalimbali mwaka 2021 na baada ya kupata matokeo haya ya utafiti, chuo kikuu kupitia wafadhili wetu ambao ni mashirika ya kimisionari yalituwezesha kifedha na kujenga Kituo cha Pamoja cha Huduma ya mkono kwa mkono kwa watoto waliofanyiwa ukatili na tayari kimeanza kutoa huduma," alisema Prof. Mapunda.

Alisema kuwa kituo hicho kinatoa msaada wa kisheria, tiba ya kisaikolojia na unasihi, matibabu ya awali pamoja na huduma za kisaikolojia na unasihi kwa wazazi na walezi na kina wataalamu wakiwamo madaktari na askari polisi kutoka dawati la jinsia la watoto.

Alisema ili kufikia malengo hayo, chuo kikuu kilianzisha mpango wa kutoa mafunzo kwa machampioni wanatokana jamii yenyewe ambao watakuwa na jukumu la kuangalia na kufuatilia kwa karibu, ili kuhakikisha watoto hawafanyiwi vitendo vya ukatili kutoka kwa wazazi wao na watu wengine.

Mratibu wa mradi huo, Virginia Bamurange, alisema licha ya kutolewa kwa msaada huo, kituo hicho kimewezesha kutoa mafunzo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari 64.

"Wako wazazi mpaka sasa hawaelewi mambo yanayowazunguka watoto wao katika zama hizi tofauti na nyakati zao hivyo ni wajibu wetu sote kutoa elimu kwa watoto wetu kuhusu namna ya kuwalea na viashiria vya visababishi vya kufanyiwa vitendo vya ukatili," alisema Virginia.

Baadhi ya machampioni waliopatiwa usafiri huo, Nuru Mtohanje, walipongeza uongozi wa chuo kikuu hicho kwa kuanzisha kituo hicho na kutambua jukumu lao kwenye mapambano hayo ya kutokomeza vitendo vya ukatili.

Naye Sagara, licha ya kukipongeza chuo kikuu hicho pia aliwataka wananchi wa wilaya ya Morogoro kujenga tabia ya kuwafichua wanaofanyia watoto vitendo vya ukatili watoto kwa kutoa taarifa polisi, ili wahusika wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

## Wakulima kicheko kupanda bei ufuta

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKULIMA wa ufuta katika wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, wamefurahishwa na ongezeko la bei ya zao hilo lililofanywa na kampuni zinazonunua, huku wakiomba kuongeza zaidi ili kupunguza gharama za uzalishaji.

Baadhi ya wakulima walionyesha furaha hiyo juzi walipozungumza na waandishi wa habari juzi wakati wa mnada wa pili wa mauzo ya ufuta uliofanyika Chama cha Msingi na Ushirika Tapwa AMCOS katika kijiji cha Singino, wilayani humo.

Wakulima hao, Salum Hemedi, Amri Yusufu, Okwi Issa na Abdallah Mbaruku, walisema wameanza kupata faraja na bei ya sasa ambayo ni Sh. 3,020 hadi 3,045 kwa kilo moja.

Aidha, walisema msimu uliopita waliuza kwa kati ya Sh. 2,000 na 2,500 bei ambayo haikurejesha gharama walizotumia kwenye kilimo.

Walisema kuongezeka kwa bei ya zao hilo mwaka huu, kutawapunguzia adha ya kuendelea kuishi kwenye umaskini kila uchao, huku wakiziomba kampuni hizo akuongeza bei kwenye mnada unaofuata.

"Kimsingi tumeanza kupata faraja kwa ufuta kupanda bei na kwa vile kuna makato unayokatwa tunaomba mnada unaofuata bei iongezeke," alisema.

Awali, Meneja wa Chama cha Ushirika Lindi Mwambao, Mohamed Swallah, akisoma matokeo ya mnada huo, alisema kampuni zilizojitokeza ni maghala ya Nangurukuru ya Kilwa, Bucco na Mtama ya Lindi na kwamba tani 4,031 na kilo 231 ziliuzwa.

# CRDB kuwajengea uwezo wajasiriamali vijana nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuendeleza jitihada zake za kuwajengea uwezo na kuwawezesha wajasiriamali vijana nchini, Benki ya CRDB imetangaza kuandaa semina maalum iliyopewa jina la 'CRDB Bank Instaprenyua'.

Semina hiyo imepangwa kufanyika Julai 16, mwaka huu, makao makuu ya benki hiyo kwa ajili ya kuwawezesha vijana ambao wanafanyabiashara kupitia mitandao ya kijamii.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Masoko cha CRDB, Joseline Kamuhanda, wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika banda la benki hiyo lililoko kwenye Viwanja vya Sabasaba mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza katika mkutano huo, Joseline alisema katika miaka ya karibuni kumekuwa na mwamko mkubwa kwa vijana kujishughulisha na shughuli za ujasiriamali hususani kupitia mitandao ya kijamii ambayo imerahisisha namna ya kuendesha biashara na kuyafikia masoko kwa urahisi.

"Vijana wamekuwa wakitumia vizuri fursa zilizoko hususani fursa za mitandao ya kijamii kufanikisha shughuli zao za ujasiriamali.

"Katika maonyesho haya tumewaona pia vijana wajasiriamali ambao wanafanya vizuri kupitia maduka mtandao, jambo ambalo limetusukuma kuwapa elimu na kuwajengea uwezo," alisema Joseline.

Alisema biashara mtandao ni moja ya eneo linalokua kwa kasi na linalopaswa kuangaliwa, ikiwa ni pamoja na kutafuta suluhu ya kuwawezesha wajasiriamali hao. Mitandao ya kijamii hususan Instagram imekuwa chachu kubwa kwa vijana wajasiriamali hapa nchini kuishi ndoto zao za ujasiriamali.

"Takwimu zinaonyesha Instagram ndiyo mtandao wa kijamii wenye watumiaji wengi zaidi duniani, wapatao bilioni 1.074, vivyo hivyo hapa Tanzania, mtandao huo unaongoza pia ndio unaongoza kwa wafuasi zaidi ya milioni 2.86.

"Hii ndiyo sababu ya kuipa jina la Instaprenyua semina hii kwani ndipo hasa vijana wengi wapo, lakini lengo ni kuwafikia vijana katika majukwaa yote ya mtandaoni," alisema.

Akizungumzia kuhusu malengo ya kuandaa semina hiyo, Mkuu huyo wa Kitengo cha Masoko alisema ina malengo makuu matano yakijumuisha kutoa mafunzo ya namna bora ya kuendesha biashara kwa wajasiriamali wanaofanya biashara mtandao na kutoa elimu ya usimamizi wa fedha katika biashara.

Malengo mengine ni pamoja na elimu ya masoko ya fedha na mitaji, na namna bora za kuyaendea masoko hayo, elimu juu ya fursa zinazotolewa na CRDB kwa wajasiriamali nchini pamoja na elimu ya urasimishaji wa biashara na faida zake kwa wajasiriamali.

CRDB pia iliutumia mkutano huo na waandishi wa habari kuwashukuru washiriki wote wa maonyesho, wafanyabiashara, taasisi, kampuni na wateja binafsi kwa kuendelea kuichagua benki hiyo kuwa mtoa huduma.

Akitoa salamu hizo za shukrani, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo na Wakati Benki ya CRDB, Bonaventure Paul, alisema msimu wa Sabasaba wa mwaka huu umekuwa na mafanikio zaidi ambapo benki hiyo imeboresha huduma zake kwa wateja na kutoa huduma kwa wateja wengi zaidi kupitia tawi maalum la benki lililoko katika Viwanja vya Sabasaba pamoja na CRDB Wakala.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko wa Benki ya CRDB, Joseline Kamhanda (katikati), akizungumza na waandishi wa habari katika tawi la benki hiyo, kwenye viwanja vya Sabasaba Dar es Salaam jana, kuhusu semina kwa wajasiriamali wanaofanya Biashara ya Mtandao "CRDB Bank Instaprenyua" inayotarajia kufanyika Julai 16, mwaka huu katika makao makuu ya benki hiyo. Wengine ni Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati, Bonaventura Paul (wapili kulia), Ofisa Mauzo wa Silent Ocean, Dotto Mayanga (wapili kushoto), Meneja Mahusiano Infucus Studio Ltd, Clair Mtui na Operesheni Meneja wa Simba Courier, James Mwambona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yajiandaa kushindana Afrika kwa kuzalisha umeme

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, amesema wamejipanga kuwa washindani barani Afrika kwa kuzalisha umeme kwa kiwango cha juu, toshelevu na kwa gharama nafuu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, mkurugenzi huyo alisema wana miradi mingi ya kuhakikisha nishati ya umeme inakuwa ya uhakika, ukiwamo mradi wa kimkakati wa Bwawa la Julius Nyerere utakaotumia maji na mingine ya gesi.

Alisema wanaamini kupitia miradi hiyo watakuwa na umeme wa kutosha, bei himilivu na kuleta ushindani katika ukanda wa Afrika. Alibainisha kuwa TANESCO ina miradi ya umeme ya kuunganisha Tanzania na nchi zingine kama Kenya, Zambia na Msumbiji na kwamba kuwapo kwa gesi ya kutosha kutasaidia kuzalisha umeme utakaowezesha biashara ya nishati hiyo na nchi nyingine.

"Tunahitaji muda na tunaamini tutafanikiwa kwa kiwango kikubwa kuuza umeme nchi jirani baada ya ndani kutosheleza.

"Uzalishaji umeme wa maji huchukua takribani miezi 36 hadi 60, tuna mipango na juhudi katika kuhakikisha tunafanikisha miradi ya namna hiyo kwa wakati ili tuwe shindani katika kanda, taifa lifanikiwe kwa kuwa na nishati ya uhakika na kwa gharama nafuu na kujenga uchumi imara," alisema.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, alisema anaridhishwa na mwenendo wa TANESCO kutokana na kukua kiufundi, uhandisi na huduma na kwamba baada ya miaka michache itakuwa moja ya mashirika bora yenye viwango vya utoaji huduma.

Pia alisema TANESCO ni shirika linalobadilika na limejipanga katika kuboresha huduma na kurahisisha upatikanaji wa umeme kwa kuusambaza kwa gharama nafuu nchi nzima, na kwamba mwelekeo wao unakwenda sambamba na bajeti ya wizara iliyowasilishwa bungeni.

"Niipongeze TANESCO kwa kuendelea kuwafikia wananchi sambamba na kupokeo kero, changamoto, maoni na kuyapatia ufumbuzi, elimu na huduma kwa umma ni muhimu kwetu hii ni namna ambavyo tumejipanga katika kuhakikisha kila mwananchi anapata na kufikiwa na huduma kwa kiwango bora zaidi," alisema Makamba.

## DCB yajivunia miaka 20 ya mafanikio yake

**Na Maulid Mmbaga**

BENKI iliyoanzishwa na Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam (DCB), imeeleza mafanikio yake kwa miaka 20 tangu kuanzishwa kwake ni pamoja na kukuza mtaji kutoka Sh. bilioni 1.7 hadi Sh. bilioni 30.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa juzi wakati wa hafla ya kusherehekea miaka 20 ya mafanikio ya benki hiyo, Mkurugenzi wa DCB, Godfrey Ndalahwa, alisema mafanikio yao mengine ni kuhuisha leseni kutoka benki ya jamii na kuwa benki kamili iliyowezesha kuhudumia wateja wadogo, wa kati na wakubwa.

Alisema wamefanikiwa kufungua matawi tisa na mawakala zaidi ya 700 maeneo tofauti nchini, kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. trilioni moja na kunufaisha Watanzania zaidi ya 400,000, kukidhi kiwango cha mtaji kinachotakiwa kisheria, ukwasi unaoridhisha na kiwango kidogo cha mikopo chechefu.

"Benki inaendelea kuboresha huduma ikihakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika, wakati tunaanza wateja walikuwa 6,530 na wameongezeka hadi kufikia zaidi ya 200,000 sambamba na ongezeko hilo la wateja pia imani yao imeendelea kuongezeka na kusaidia amana nazo kukua.

"Mwaka 2021 benki ilifanikiwa kukuza mikopo yake hadi kufikia Sh. bilioni 121 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 16 kwa mwaka, na imeweza kupunguza mikopo chechefu kutoka asilimia 11.6 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 7.3 mwaka 2021," alisema Ndalahwa.

Aliongeza kuwa benki hiyo imefanikiwa kukuza amana za wateja mwaka hadi mwaka na kufikia Sh. bilioni 125 Desemba 2021, huku wakiwa na malengo ya kufikia Sh. bilioni 162 mwisho wa mwaka huu.

Vilevile, alibainisha baadhi ya vikwazo ni mikopo chechefu kuwa katika kiwango cha juu, ukwasi usioridhisha kwa maendeleo ya benki pamoja na kujiendesha kwa hasara.

Pia alibainisha malengo yao kutoka mwaka 2020 hadi 2025, ikiwamo kuongeza kiwango cha faida kinachopatikana kila mwaka hadi kufikia Sh. bilioni 11.

Alitaja vipaumbele vyao ikiwamo kukuza kiwango cha mikopo kwa wateja kutoka Sh. bilioni 104 mwaka 2020 hadi kufikia Sh. bilioni 290 mwaka 2025 na kuongeza mapato yasiyotokana na riba kutoka asilimia 26.4 hadi 35.

Vingine ni kuongeza mchango wa amana za gharama nafuu katika amana zote za benki kutoka asilimia 34 mwaka 2020 hadi kufikia 60 ifikapo 2025, kukuza mtandao wa DCB kwa ufanisi na kuongeza wigo wa mikopo itolewayo kidijitali hadi kufikia asilimia 50.

# Shandong wajivunia kushiriki maonyesho biashara Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

MAONYESHO ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Tanzania, maarufu Sabasaba, yanafanyika Dar es Salaam, kampuni zaidi ya 1,800, taasisi za serikali na mashirika ya kijamii kutoka nchi 32 za Afrika, Asia, Ulaya na Columbia zikishiriki.

Maonesho hayo ni makubwa zaidi Tanzania na ni moja ya maonyesho muhimu ya kibiashara nchini na hata katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki yanayodhihirisha wigo wa bara zima la Afrika.

Kama washirika wakubwa wa kibiashara wa Tanzania, kampuni za biashara ya China zimeshiriki katika maonyesho hayo. Jimbo la Shandong, China, likiwa na kampuni zaidi ya 50, limeshiriki katika maonyesho hayo muhimu na kuwa kivutio kikubwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Biashara na Usafirishaji Afrika Mashariki (EACLC), Cathy Wang, alibainisha jana kuwa jumla ya kampuni 53 za Shandong zimeshiriki katika maonyesho hayo, zikihusisha biashara ya kimataifa, maendeleo ya majengo, vifaa, mashine za kilimo, nguo, vifaa vya ujenzi, ufugaji, kilimo na bidhaa zingine.

Alisema wateja kutoka Afrika wanaweza kufurahia bidhaa za ubora wa hali ya juu zinazotengenezwa Shandong na kutoa fursa za ajira za ndani na kodi, pia wameweka msingi mzuri kwa kampuni za biashara za Shandong kufungua soko la Afrika na kufanikisha ushirikiano.

Wakati wa maonyesho hayo, mratibu wa Jumba la China Shandong Pavilion, Weihai Huatan Supply Chain and Management Co. LTD, alishirikiana kwa kina na Taasisi ya Confucius ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kutengeneza mwonekano mzuri wa banda Shandong, kukiwa na dansi ya joka na onyesho la ngoma ya simba kuleta utamaduni wa China barani Afrika, maonyesho yaliyovuta hisia za mamia waliotembea banda hilo.

Julai 4, mwaka huu, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alitembelea Banda la Shandong kwa ajili ya kukagua eneo hilo na kuridhishwa na kazi zao.

Kwa mujibu wa Wang, Hhdi kufikia Julai 6, banda la China Shandong lilipokea wateja zaidi ya 1,500. Alisema banda la China Shandong litakaribisha wafanyabiashara wengi kutoka Tanzania na nchi jirani ili kusukuma mabadilishano ya biashara.




Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Biashara M-Pesa, Tulisindo Mlupilo (watatu kulia), akimwekea mafuta dereva wa bodaboda, Ali Juma, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya M-Pesa Imeitika katika eneo la Manzese, Dar es Salaam jana, ikihusisha huduma ya wese activation, ambapo madereva 125 wa bodaboda walipata ofa ya kuwekewa mafuta bure wanapolipa kwa M-Pesa. Wengine ni Mkurugenzi wa Udhibiti wa Hatari na Utii wa Sheria Vodacom Tanzania Plc, Agapinus Tax (wa pili kulia) na (kulia) ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Digitali na huduma za ziada wa kampuni hiyo, Nguvu Kamando. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UCSAF sasa yafikisha mawasiliano kata 830

**Na Mary Geofrey**

MFUKO wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umefikisha huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo yasiyo na huduma katika kata 829 kati ya 1,234 zilizoainishwa.

Mtendaji Mkuu wa Mfuko huo, Justina Mashiba, alibainisha hayo juzi jijini Dar es Dalaam katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mfuko huo mwaka 2009 hadi mwaka huu, wamefikia kata hizo katika kuwawezesha wananchi kufikiwa na huduma za mawasiliano nchini.

Vilevile, alisema wanatekeleza mradi wa usikivu wa Redio ya Taifa na redio za kijamii katika baadhi ya maeneo nchini hususani mipakani, yasiyo na huduma hiyo na yenye huduma hafifu.

"Kwa kushirikiana na TBC, mfuko umekamilisha ujenzi wa studio za redio jamii Dodoma na Arusha pamoja na vituo vitano vya kurushia matangazo ya redio TBC Taifa na TBC FM," alisema.

Mtendaji Mkuu huyo alisema vituo hivyo vimejengwa Kisaki na Mlimba mkoani Morogoro, Ngara mkoani Kagera, Ruangwa mkoani Lindi na Ludewa mkoani Njombe kwa lengo la kudhibiti kutumia mawasiliano ya nje ya nchi.

Alisema pia wameanzisha kituo cha miito ya dharura Zanzibar ili kuiwezesha serikali kuwa na kituo cha kuratibu taarifa za matukio ya dharura ikiwamo moto, ajali na mlipuko wa magonjwa.

Mashiba alisema pia wameunganisha shule za umma kwenye intaneti kwa kuzipatia vifaa vya TEHAMA kwa lengo la kuwawezesha kujifunza kupitia vifaa hivyo katika hatua za awali.

"Hadi sasa jumla ya shule 811 zimepatiwa vifaa zikiwamo kompyuta na printa," alifafanua.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, baada ya kutembelea banda hilo, alipongeza mfuko huo kwa juhudi kubwa unazofanya za kusambaza huduma za mawasiliano kwa wote.

Alisema juhudi hizo zinatakiwa kuendelezwa ili kufika katika kata zote na maeneo ambako hakuna mawasiliano ili Watanzania wote wanufaike na huduma hiyo nchini.

# Banda la bidhaa za China lawavutia wengi Sabasaba

**Habari zote na Elizabeth Zaya**

MAMIA ya wananchi jana walimiminika katika banda la bidhaa za watu wa China lenye bidhaa kutoka Jimbo la Shandong kuangalia bidhaa na kujifunza utamaduni wao.

Nipashe ilishuhudia makundi mbalimbali yakiwamo ya watu wazima, vijana na watoto wakimiminika katika banda hilo ambalo pia mlangoni lilikuwa limepambwa kwa burudani za vinyago vinavyoonyesha utamaduni wa China.

Nipashe ilizungumza na baadhi ya wananchi waliokuwa wakitembelea banda hilo ambao walisema miongoni mwa vitu vinavyowavutia ni bidhaa zilizomo katika banda hilo.

Ashrafu Omari alisema alichovutiwa kwenye banda hilo ni nyasi bandia, vifaa vya ujenzi ikiwamo marumaru, vipuri vya magari, viatu na vitenge vya kichina.

"Kilichonivutia kwenye banda hili kwanza ni vifaa vya ujenzi, mashine ya kukoboa na kusaga, samani za ndani na marumaru kwa sababu vinaonekana ni imara sana, na pia kuna utamaduni fulani unavutia," alisema Omari.

Nipashe ilizungumza na Mkurugenzi Mkuu ambaye taasisi yake ndiyo inaratibu kampuni za kichina kutoka Jimbo la Shandong linalojulikana kama East Africa Commercial and Logistic Center, Cathy Wang.

Mkurugenzi huyo alisema ma jumla ya kampuni 52 kutoka China zimeshiriki katika maonyesho hayo ya 46 ya Sabasaba kwa ajili ya kuonyesha bidhaa na utamaduni mbalimbali wa watu wa China.

Alisema lengo kuu la kushiriki maonyesho hayo ni kuimarisha na kudumisha ushirikiano baina ya nchi hizo mbili.

"Tanzania na China wamekuwa wakishirikiana katika mambo mengi na ndiyo maana inapokuja vitu kama hivi, tunajitoa kushiriki ili kuendeleza urafiki na ushirikiano wetu," alisema Wang. Alitaja bidhaa zingine ambazo zimo katika banda lao kuwa ni marumaru za mbao, samani za ndani na nguo.

Alisema wapo katika maonyesho hayo mpaka mwisho na kuwaalika wananchi kwenda kuwatembelea na kujifunza mambo mbalimbali.

Katika maonyesho hayo, jana idadi watu iliongezeka kutembelea mabanda mbalimbali kuanzia asubuhi.




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje Ushirikiano wa Kimataifa na Afrika Mashariki, Balozi Fatma Rajab, akisaini kitabu cha wageni wakati alipotembelea banda la maonyesho la kampuni ya Barrick Sabasaba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yakunwa na ubora Sabasaba

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi(CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema chama hicho kimeridhishwa na namna ambavyo Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), yalivyoboreshwa.

Akizungumza alipotembelea maonyesho hayo ya 46 yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba, Shaka alisema wanaamini wafanyabiashara wa Tanzania sasa watafanya vizuri katika kushindanisha bidhaa zao kimataifa.

"Mafanikio haya ya kibiashara yanayoonekana sasa kutokana na nia njema ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kufungua milango ya fursa kwenye sekta mbalimbali ambazo zinagusa wananchi moja kwa moja," alisema Shaka.

"Ameondoa vikwazo na tozo mbalimbali ambavyo vilikuwa vikiwakwamisha wafanyabiashara nchini kushindwa kuendesha shughuli zao hizo kwa uhuru, hili ni jambo jema sana," alipongeza.

Alisema ni lazima wakiri kwamba sekta ya biashara ilidorora na hata kuchangia mzunguko wa fedha kuwa mdogo na kwamba uamuzi wa serikali kuondoa vikwazo hivyo utarudisha kwa kasi na ari kwa idadi kubwa ya wafanyabiashara kuingia huko.

"Na ndiyo maana hata maonyesho ya mwaka huu yamefanikiwa sana, kwa namna walivyoyaandaa, mwitikio wa ushiriki kwa wenyeji na wageni na huduma mbalimbali zinazopatikana humu, vyote vinaleta faraja kubwa sana.

"Na tumekuta ubunifu mkubwa sana ambao umefanywa na wafanyabiashara wetu wa ndani, kwa hiyo sisi kama chama tumeridhishwa sana na tunawapongeza pia Mamlaka ya Usimamizi wa Maendeleo ya Biashara (TANTRADE) kwa kazi kubwa ambayo wamefanya," alisifu.

Shaka alisema wana imani idadi ya wafanyabiashara wanaokuja kutafuta fursa mbalimbali za kuwekeza Tanzania, itazidi kuwa kubwa kutokana na wengi wao kuvutiwa na kazi iliyofanywa kutokana na filamu ya Tanzania The Royal Tour.

## Nape apongeza TTCL utekelezaji maagizo

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amelipongeza Shirika la Mawasiliano (TTCL) kwa kutekeleza maagizo yaliyotolewa na serikali ya kupunguza matumizi ya serikali kwa kufanya mikutano kwa njia ya video.

Nape alitoa pongezi kwa shirika hilo alipotembelea katika banda lake kwenye viwanja vya Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea kwenye Viwanja vya Sabasaba na kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na Mkurugenzi wa Biashara wa mamlaka hiyo, Vedastus Mwita akiwa jijini Dodoma.

Nape alisema matumizi ya TEHAMA kwenye shughuli mbalimbali za serikali yatasaidia kuleta matokeo chanya kwa serikali hiyo.

"Ninafurahi kuona kwamba mmeanza kutekeleza agizo la serikali la kuipunguzia gharama kwa kufanya mikutano kupitia video, tunataka kuona jambo hili linaleta matokeo chanya kwa serikali," alisema Nape.

Mkurugenzi huyo wa TTCL, Mwita alisema watahakikisha wanatekeleza agizo hilo la serikali kwa kutumia TEHAMA katika kuendesha mikutano yake.

## Mtaalamu awapa mbinu wakulima kukabili sumukuvu

MTAALAMU kutoka Wizara ya Kilimo amewataka wakulima kufuata kanuni bora za kilimo ambazo wanapatiwa na wataalamu wa kilimo ili kuepuka kuzalisha chakula chenye sumukuvu.

Mercy Buta, Mtaalamu wa Sayansi na Usalama wa Chakula kutoka wizara hiyo, alitoa kauli hiyo juzi kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba.

Alisema kuna athari nyingi zinazotokana na wakulima kutokufuata kanuni bora za kilimo ambazo huwapata walaji wa mazao yatokanayo na kilimo.

"Wakulima wafuate kanuni bora za kilimo ikiwamo kupanda kwa nafasi, kupalilia kwa nafasi, kupanda mbegu bora ambazo zimethibitishwa na kuvuna kwa wakati," alisema Buta.

Aliongeza: "Sasa hivi kuna kiuatilifu cha kibaiolojia ambacho kimetengenezwa A to Z ambacho kimepandikizwa kuvu ambao ni salama kwa maisha ya binadamu. Yamepandikizwa ili unapokwenda kumwagia shambani wenyewe wanapambana na wadudu wabaya ambao wanazalisha sumukuvu."


Pia alisema kwa kufuata kanuni bora za kilimo zinasaidia kuwawekea mazingira magumu ya ukuaji wadudu hao wa sumukuvu.

"Ukiweza kudhibiti hapo, kwenye kuvuna vilevile ukifanyika kwa wakati bila kumwaga mazao shambani na kusubiri baada ya muda fulani ndio unakwenda kubeba siyo sahihi, unatakiwa uvune kwa wakati sahihi ili mazao yasiloweshwe na mvua na kusababisha tatizo hilo.

"Vilevile, unapokwenda kukausha unatakiwa ufanye hivyo ukiwa umeweka turubai ili mazao yasiguse udongo kwa sababu hao kuvu wanaishi huko, kwa hiyo lazima tufuate ukaushaji bora," alisema.


Ukurasa 12

Nyayo za TASAF Singida zilivyowaletea ahueni wakazi wake, kila mmoja na yake



Ukurasa 13

Suala posho kwa wafungwa tulitafakari kwa kina chake


Ukurasa 14

MJADALA MOTO, MAJIBU YA UMMA...

**Hoja mikopo asilimia 10, faida zake na darasa wabunge, 'serikali sikivu'**

BUFE

IJUMAA JULAI 8, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Ubia wa ubinifu katika ujasiriamali na teknolojia 'unavyowatoa' vijana

**Na Urio Fredy,** SJMC

KUNA nadharia ya kijamii imedumu muda mrefu, kwamba aliye mvivu anakula kwa tabu na mateso, lakini mwenye nguvu mwilini na ukakamavu, anakula vizuri baada ya kufanya kazi za mikono yake.

Leo hii katika zama za sayansi na teknolojia, hata kama mtu ana nguvu nyingi, nadharia hiyo sasa inaboreshwa nafasi ya nguvu inaongezwa pia teknolojia na akili binafsi, vyote vinazaa ufanisi na tija inayoshamiri.

Sasa kuna swali kuhusu usemi "mtaji wa masikini ni nguvu zake mwenyewe" una nafasi gani hapo? Kimsingi, imedhihirika kwamba mafanikio ya kiuchumi na kibiashara yanategemea sana mchango nafasi ya mwili, maarifa yake na nyenzo teknolojia.

Si mbaya lugha ya maboresho ikawa katika sura ya matamshi: "Mtaji wa masikini ni ubora wa maarifa yaliyowekezwa au kutekelezwa."



Shughuli za ujasiriamali zikiendelea. **PICHA: MTANDAO**

Daima maarifa sahihi ni yanayomuwezesha mtu kupata kile anachokihitaji, kupitia hekima aliyojiongezea katika nia ya kuweza kumudu mazingira yanayoweza kukwamisha malengo yake.

Maarifa yanapotumika pamoja na nguvu ndogo ya mwili humuwezesha mjasiriamali au mfanyabiashara kufanya biashara kwa mafanikio katika mazingira yanayobadilika.

Kujitangaza au kutafuta masoko ya bidhaa au huduma kimtandao, ni hali inayoshika kasi sasa, ikiwa rahisi na inatumia gharama nafuu kuwafikia wengi zaidi na kwa muda mfupi.

Mjasiriamali anaingia katika masharti, kwamba jambo linalotakiwa sasa ni kuzingatiwa matumizi sahihi ya mitandao, badala ya kuitumia kuweka vitu visivyo na msingi wa kusaidia kuleta maendeleo.

Safari inakoelekea ni kuhitaji ujuzi mpya kidijitali, ubunifu wa kufikiri, kutatua matatizo, ushirikiano, uelewano na kubadilika kutokana na mazingira au nyakati.

Sababu kubwa ya kutumia masoko kidigitali, inaangukia katika kutangaza bidhaa au huduma ili watu waweze kuzifahamu, pia kutoa taarifa juu ya biashara na huduma katika jamii hata kuweza kuziuza na kutengeneza faida.

Hadi sasa katika jamii, kuna mitandao mingi ya kijamii nchini, inayomfanya kila mjasiriamali anapaswa kujiunga nayo kuweza kuwafikia wateja wengi zaidi katika kukuza biashara, hali kadhalika masoko ya bidhaa na huduma anazouza.

Katika uhalisia, inaonekana hali ya kutapakaa mtandao kama vile Baruapepe, Blogu na kurasa za kijamii kama vile; Facebook, Instagram, WhatsApp na Twitter, kote ni maeneo ya mitandao kijamii, wanakotumia watu wengi zaidi. Hivyo, kuna njia rahisi za kuwafikia wateja kwa wakati mmoja, pamoja na kutengeneza wateja wapya

### KAULI ZA KITAALAMU

Mshauri wa masuala ya biashara aitwaye, Peter Asenga, anahimza matumizi ya intaneti na mitandao ya kijamii na hasa instagram kwa vijana wa leo, inawafaa na kuwapa fursa ya kujiajiri na wakajikwamua, anausifu mtandao wa instagram una nguvu kubwa katika jamii, hivyo una nafasi ya kutumiwa zaidi.

Ushauri wake ni kwamba, kijana anaweza kutumia fursa hiyo kwa kujitangaza au kutangaza bidhaa na huduma zake, akawafikia watu wengi kwa muda mfupi sana.

Pia, anazungumzia tabia ya vijana wengi wa sasa kukosa udhubutu wa kufanya akisisitiza ndio ufunguo wake, ukiendana na ubunifu katika ujasiriamali kwa namna itakayowavutia wateja wengi.

Anasema, vijana wengi wanaigana katika mawazo ya biashara, kinyume na wanachopaswa, kufanya ubunifu katika biashara au wazo lake, ili kuwavutia watu wengi kutafuta huduma wanayoitoa.

Dk. Darius Mukiza, Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC), anakoongoza kitengo cha Uhusiano kwa Umma na Masoko, anawataka vijana a hasa wasomi wa vyuo vikuu kutumia taaluma zao kuwabadilishia maisha.

Mhadhiri huyo anawahimzia wasomi vyuoni kutumia stadi zao kuwaletea mabadiliko kimaisha, wakiepuka kuwa sehemu ya wimbi la vijana wahitimu vyuoni, wanalundikana kusubiri ajira, badala ya kutumia fursa kiganjani.

Akiwa mahsusi anarejea mitandao, anawaasa wanafunzi wake SJMC, kutumia fursa ya mitandao ya kijamii kuwainua kama vile; youtube channel, instagram, blogs kuwabadilishia maisha, huku wakioanisha na taaluma zao kutoka vyuoni, ikawa fursa ya kujikwamua kiuchumi. Hapo mwanazuoni huyo anatumia mifano hai iliyoko, kuwa sehemu ya kujifunza.

UCHUMI

# Nyayo za TASAF Singida zilivyowaletea ahueni wakazi wake, kila mmoja na yake

**Na Elisante John,** Singida

## • Simulizi: Wanamudu mlo, mitaji ipo na nyumba wanajenga

SEHEMU ya mikakati ya kusaidia jamii, kuondokana na adha ya umasikini nchini, kitaifa kumeanzishwa chombo maalum kuukabili, huo ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, maarufu kama 'TASAF.

Katika utendaji wake, nayo imeanzisha mradi wa kuzipatia fedha kaya masikini zaidi kwa lengo la kuzikomboa kiuchumi na kuzijengea uwezo wa kumudu maisha yao.

Wilaya ya Singida, ni kati ya halmashauri saba za mkoa zinazonufaika na Tasaf, kutokana na kaya 7,138 zenye walengwa 5,839 waliotambuliwa na sasa zinanufaika na mpango huo, hadi kufikia mei mwaka huu.

Mratibu wa TASAF katika halmashauri hiyo, Piyazis Tindikali, anasema mpango huo ulianza Aprili 2014 ukiwa na kaya 8,132, lakini mpaka kufikia Mei 2022, kuna vijiji 84 vimeingizwa katika mpango wa kunusuru kaya masikini zaidi, kutoka vijiji 40 vya awali.

Anasema katika mwaka wa fedha 2021/2022, halmashauri ilipokea zaidi ya Sh. bilioni 1.2/-, ikizielekeza katika malengo yaliyokusudiwa, ikiwemo ajira za muda zinazotokana na malipo ya ujira Sh. 3,000/- kwa siku kwa walengwa wa mpango.

Tindikali anafafanua, kwamba, kutoka mwaka 2014 hadi Mei mwaka huu, halmashauri ilipokea zaidi ya Sh. bilioni 17.1/- kutoka serikali kuu kupitia Tasaf, zilizotolewa na mpango wa awamu ya tatu wa mradi (TASAF-III).

"Fedha zote hizi zimesaidia walengwa, kupitia miradi mbalimbali, kama vile ruzuku ya kutimiza masharti ya afya na elimu, ajira za muda, ujenzi wa miundombinu na mradi kwa wasichana, wa 'timiza malengo' wameanzisha pia vikundi vya kiuchumi," anafafanua.

Anaeleza, kwa sasa mpango huo umeimarishwa na kuboreshwa, mahudhurio kwa watoto yako 11,069 wanaotimiza masharti ya elimu, huku wengine 2,114 wanaotimiza masharti ya afya, wananufaika na kliniki wakiboresha afya zao.

Anafafanua, suala la uhalalishaji fedha kwa kaya msikini zinazokidhi masharti ya elimu na afya ulioanza Septemba 2014, umeziwezesha awamu 39 za malipo kwa walengwa hadi kufikia mei mwaka huu, hata kuleta mapinduzi kiuchumi kwa kaya husika.

### WANUFAIKA WAKOJE?

Baadhi ya wanufaika, akiwemo Joyce Mpanda (57) wa kijiji cha Ngamu, kata ya Mwasauya katika,



Sura pana ya manufaa ya TASAF, mkoani Singida, kuanzia makazi, ufugaji ng'ombe na kuku, zilizotolewa ushuhuda katika Halmshauri ya Wilaya ya Singida. **PICHA ZOTE: MATANDAO**

> **"Nimenunua mashine ya kusaga kahawa, yenye thamani ya Sh. 55,000, kwa ajili ya kurahisisha shughuli zangu, huku pia nikiongeza mifugo.**



Halmashauri ya Wilaya ya Singida, anasema Tasaf, imempatia uwezo wa kuyabadili maisha yake, ikilinganishwa na alivyokuwa awali.

Anasema maisha yake awali yalikuwa magumu, mashaka makubwa na kubahatisha, huku milo mitatu kwa siku ikimshinda, lakini hivi sasa anajigamba mambo yamemnyookea.

Pia anataja kabla ya kujiunga na TASAF mwaka 2014, hakuwa anajishughulisha na mradi au kazi yeyote ya Kiuchumi, akitaja sababu ni kukosekana mtaji, hali iliyoathiri maendeleo ya pamoja na familia.

"Hali niliyokuwa nayo mwanzo, ilinisababishia kukosa hata akiba ya chakula na kumudu mlo wa siku...sikuwa kabisa na uwezo wa kusomesha watoto wangu kutokana na kuyumba kwa uchumi," anafafanua.

Kwa mujibu wa Joyce, baada ya kujiunga na TASAF, alianza kuweka akiba na hatimaye akapata mtaji uliomuwezesha kufungua biashara ya kinywaji cha asili aina ya Togwa na kufuga kuku wa asili.

Anasema, pia kwa kushirikiana na familia yake, alijenga nyumba ya kisasa yenye vyumba vitatu kwa kutumia matofali ya kuchoma, akiezeka kwa bati, akaunganisha nishati ya umeme inayotokana na jua.

"Mimi na mume wangu Charles Ng'aida, ni wanufaika wa TASAF, tumejenga nyumba hii tunayoishi, kama unavyoiona hapa...tunafuga kuku wa asili na hivi sasa hapa nilipo, ninafuga kuku zaidi ya 30," anasema Joyce.

Mama huyo anataja mpango wake wa siku zijazo ni kupanua zaidi shughuli zake za ujasiriamali, ili aongeze kipato cha kaya na kusomesha watoto, kwa lengo la kuwajengea uwezo kumudu maisha yao ya baadaye.

Mnufaika Mzee Daniel Kessy (74), ana simulizi yake kwamba amefungua biashara ya genge kupitia nguvu ya TASAF, akiwa kijijini Ngamu kata ya Mwasauya, katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Anafafanua awali familia yake haikuweza kupata milo mitatu, wala akiba ya chakula, lakini hivi sasa ana uhakika wa milo mitatu.

Kwa mujibu wa Mzee Kessy, alipoanza kupokea ruzuku, alianza na mkakati kutumia kidogo anachopokea kwa ajili mtaji wa biashara ya genge, iliyomsaidia kumuinulia kipato hadi akawa na akiba ya chakula na kumsomesha mmoja wa wajukuu wake.

Katika biashara hiyo, anauza bidhaa za viwandani na shamba, na kwa kushirikiana na mke wake, aliyemtaja kwa jina la Mwanaidi Ibrahimu.

Katika malengo yake, Kessy anasema, atahakikisha kupitia biashara ya genge ataimarisha kwa kuongeza bidhaa, ili kupata duka kubwa lenye bidhaa tofauti tofauti na kuziuza kwa bei ya rejareja, akitanguliza shukrani kwa TASAF.

Mwanahamisi Shomari (49), naye anajivunia ruzuku ya TASAF imewaboreshea huduma, katika kijiji cha Itamka ya Mrama, akibadili maisha kutoka makazi kwenye nyumba ya Tembe, hadi ya kisasa, watoto wake wakipata mahitaji muhimu ya shule.

Anasimulia alipoanza kupata ruzuku, alimaliza tatizo la chakula, kisha akapata mtaji wa kuuza samaki na bagia, matokeo yake sasa anamudu milo mitatu, kujishughulisha na ujasiriamali, ikiwemo ufugaji kuku na kuuza samaki.

Mwanahamisi anasema, sasa anajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula na biashara, hasa zao la alizeti, vyote vikimboreshea kipato cha familia yake.

Zainabu Ng'aioa (51), ni mwanamke anayenufaika na ufugaji wa mbuzi katika Kijiji cha Unyampanda, kata ya Mughunga, kutokana na ruzuku ya TASAF, anasema baada ya kupata fursa hiyo mwaka 2016, akaweza kukusanya fedha za ruzuku, kisha akanunua mbuzi wanne wa kufuga.

Mwanamama huyo anafafanua kwamba, mbuzi hao baada ya kuzaliana, baadhi aliwauza na kufanikiwa kununua mabati 30 aliyoyatumia kufunika nyumba ya kisasa aliyoijenga kwa kutumia matofali ya kuchoma, hivyo akaondokana na adha ya kuishi kwenye nyumba ya tembe.

Pili Mohamedi (44); ni mnufaika wa TASAF, anayeishi kijijini Ilongero, anasimulia kwamba baada ya kupata nafasi hiyo, aliitumia kwa kujenga nyumba bora ya bati, iliyogharimu mabati 31 na matofali 1,600 ya saruji.

Anasema, sasa ameweza kumudu gharama ya umeme baada ya kugharamia matengenezo ya mfumo mzima wa nishati hiyo katika nyumba yake (wiring) iliyomgharimu Sh. 220,000, lakini bado anasubiri kuunganishiwa na mamlaka husika (Tanesco).

Pia, anataja kujiunga na moja ya kikundi ambacho walengwa wa mpango huo wamekianzisha na kukipa jina la 'mkombozi', kilichopo kijiji cha Ilongero, kwa ajili ya kujiwekea akiba na kukopa.

Pili anasema, kupitia fedha za ruzuku na akiba anayojiwekea kwenye kikundi kimemhakikishia kupata mtaji wa kufungua mgahawa, anaoutumia kuuza vinywaji mbalimbali, ikiwemo kahawa, tangawizi na alkasusi.


Pili anasema, amenunua mashine ya kusaga kahawa, yenye thamani ya Sh. 55,000, kwa ajili ya kurahisisha shughuli zake, huku pia akiongeza mifugo.

Anafafanua kuwa, malengo ya baadae ni kuboresha zaidi hali yake kiuchumi, kupitia maboresho anayoendelea kuyafanya kupitia biashara yake ya mgahawa, ufugaji kuku, mbuzi, ng'ombe na kuongeza uzalishaji wa mazao ya shamba.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Singida ina watu 225,821, wakiwemo wanawake 113,749 sawa na asilimi 50.4, wanaume 111,772 asilimia 49.6.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Suala posho kwa wafungwa tulitafakari kwa kina chake






NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

KUNA wakati binadamu anaweza kusikia jambo asiliamini, lakini kumbe likawa la kweli akabakia anajisemea tu moyoni, kuwa pengine dalili za mvua ni mawingu au lisemwalo lipo kama halipo, linakuja.

Nami nilisikia hivi karibuni kuwa nchini kuna mpango wa kuanza kulipa posho wafungwa, ili wamalizapo kifungo chao, basi angalu wawe na kitu kidogo cha kuanzia maisha.

Nilijiuliza kama nimesikia kweli au pengine, ni ndoto iliyotokana na filamu niliyoiangalia kwenye televisheni ikihusu maisha ya wafungwa Ughaibuni! Kumbe ilikuwa ni uhalisia kabisa.

Juzi kati hapa nikathibitishiwa na tukio lililofanyika wilayani Ludewa, ambako Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana alitoa mizinga ya nyuki kwa ajili ya gereza la Ludewa.

Mkuu wa gereza hilo akipokea msaada huo, akawaambia wanahabari kuwa anaipongeza serikali kupitia wizara hiyo kwa kutoa mizinga hiyo itakayosaidia kuwa mradi wa kuingiza kipato kwa gereza na kuwezesha kupata fedha zitakazolipa posho za wafungwa.

Kwangu mimi mpaka sasa likawa fumbo lisilo na ufumbuzi, kwamba sasa wafungwa watakuwa wanawekewa posho zao, ili mwisho wa adhabu zao basi angalau wawe na kitu cha kuanzia maisha.

Ndiyo, ni wazo zuri kama ilivyokuwa huko nyuma, kwamba wafungwa wapewe mafunzo ya ufundi na wamalizap kifungo chao, basi ikiwezekana wapewe zana ili warudipo uraiani, waanzishe viwanda vidogo au wajishughulishe na kitu cha uzalishaji mali.

Hiyo ni kwa nia njema ya kuona kuwa wanabadilika tabia na kupata kitu cha kufanya na hivyo kuondokana na makundi na vitendo vya kihalifu katika jamii na kuishi kama raia wema. Sina uhakika kama lilifanyika au linafanyika.

Narudia, ni nia njema sana inayojali utu wa mtu, inayotambua kuwa binadamu anaweza kukosea na akajirekebisha baada ya muda fulani na kurejea hali ya kawaida na kuishi vizuri tofauti na tabia za awali zilizomwingiza matatizoni.

Kwa kuamini hili, ndiyo sababu kwa wenzetu wa Zanzibar, magereza yanaitwa vyuo vya mafunzo, kwamba aingiaye humo,hata kwa kuua anakwenda kupata mafunzo ya kurekebisha tabia na kurejea kuwa raia mwema.

Tunaweza kuita hivyo, lakini kinachofanyika humo kinaweza kisioane, maana kuna hukumu mathalan: Kifungo cha Maisha Jela na Kazi ngumu.

Huyu mhalifu anapokuwa amethibitishwa kufanya uhalifu na kuhukumiwa adhabu ya kifungo jela na huko akaenda kulipwa posho, sioni kama inakaa sawa.

Ni kwa sababu itakuwa ni kichocheo cha wengine kwenda kuzitafuta posho hizo na njia ya kufika huko inajulikana. Ila kuna swali, afungwaye maisha inakuwaje na hiyo posho?

Tumekuwa tukishuhudia viongozi wakuu wa nchi yetu, wakitoa misamaha kwa wafungwa na kurudi uraiani, lakini kabla hawajazoea uraiani, baadhi yao hurudia au kufanya mengine na kurudi kifungoni.

Pia, tumekuwa tukishuhudia katika muktadha huohuo, wafungwa wakisamehewa na baadhi yao kukataa kutoka magerezani! Kwanini? Kwa sababu huko ndiko yaliko maisha bora kwao, kuliko uraiani.

Kwa sababu, huko ndiko wanapata mlo bure na malazi bure. Sasa iweje umtoe huko umrudishe uraiani kuanza maisha ambayo hakuyazoea na lakini hana cha kufanya? Anaona bora akae huko huko.

Ukimpa fedha za kianzio, ataanza mradi gani katika mazingira kama haya na asione bora kurudi tena ndani kuendelea kusaini posho? Hata mimi nitafanya hivyo, ni kujihakikishia maisha ya ndani yenye posho isiyonunua kitu ila mtaji wa kumaliza kifungo.

Maana yake, ni sawa na kumpa mtu tuzo au cheti cha kumaliza mafunzo, kwamba sasa wewe umehitimu mafunzo humu jela, chukua hiki kikakutambulishe na kukusaidia maishani.

Tukiendelea na uamuzi huu, bila shaka kuna siku tutaamua wafungwa wawe wanapelekwa Coco Beach, kwa walio jirani Dar es Salaam au kuwasogeza katika hoteli za kisasa.

Tusiendekeze mambo haya, mfungwa ni mfungwa tu, ingawa bado ana utu na ubinadamu wake. Kumlipa posho wakati askari Magereza anayemlinda mshahara wake ni wa kijungu jiko, haitaeleweka. Kodi ya wananchi isichezewe, tutafakari hili kwa kina. Alamsiki!

UCHUMI

MJADALA MOTO NA UTETEZI WA HAKI YA UMMA...

# Hoja mikopo asilimia 10, faida zake na darasa wabunge, 'serikali sikivu'

**Na Mwandishi Wetu**

MIONGONI mwa mijadala iliyochukua nafasi kubwa kwenye Bunge la Bajeti lililomalizika hivi karibuni, ni mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa makundi maalumu ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Mikopo hiyo ambayo hutolewa na halmashauri zote nchini kutoka kwenye mapato yake ya ndani, imekuwa msaada mkubwa kwa makundi hayo katika kuanzisha shughuli za uzalishaji mali.

Inafahamika kwamba wapo Watanzania wengi ambao wamefanikiwa kuanzia biashara kupitia fedha hizo za masharti nafuu na baadaye kuwa sehemu ya watu wanaochangia ukuaji wa pato la taifa.

Hatua hiyo ya serikali inalenga kuhakikisha kuwa makundi maalumu yakiwamo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambayo yamekuwa yakikabiliana na changamoto za kiuchumi, hayaachwi nyuma kwenye ushiriki wa ukuaji uchumi.

Hiyo ni kwa sababu mifumo iliyopo ya kitamaduni na kimazingira inawanyima fursa za ajira, kipato na wakati mwingine sauti zao zinaminywa na sasa makundi hayo yamekuwa kipaumbele kikubwa serikalini.

Katika mjadala huo wa bunge, wapo waliopinga hatua ya serikali kutaka kupunguza fedha hizo kutoka asilimia 10 hadi tano, ikiwa ni mkakati wa kuwahuisha pia wafanyabiashara wadogo (Machinga) kuwa sehemu ya wanufaika wa mpango.

Baada ya mjadala mrefu, serikali ilisikia kilio cha wabunge na kuridhia kuendelea nayo, lengo ni kuwawezesha wananchi kushiriki kwenye ukuaji huo wa uchumi.

Akizungumza bungeni katika kikao hicho kilichomalizika siku kadha zilizopita, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema serikali imeendelea kutekeleza azma ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali.

Hapo anaitaja ni kuanzishwa vituo maalum vya uwezeshaji, utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi na kutekeleza mpango wa kunusuru kaya masikini.

Hadi Februari mwaka huu, serikali kupitia mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi imeshatoa mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Sh. 631 bilioni kwa wanufaika 1,194,155.

Pia, imeanzisha vituo 17 vya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Singida, Rukwa, Kigoma na Dodoma ambayo tayari matunda yake yameanza kuonekana.



Wajasiriamali kinamama vijijini wakiwa katika majukumu yao ya kiuchumi. Mikopo ya halmashauri ni sehemu muhimu ya nguzo yao ya mitaji. **PICHA: MTANDAO**

> **Hii hatua ya kutujengea uwezo ni uamuzi wa kupongezwa kwani kupitia mafunzo haya makandarasi wanapata uzoefu na ujuzi wa kujaza mikataba na kutekeleza.**

Eneo lingine ambalo limekuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi ni mikopo ya asilimia 10 inayotokana na makusanyo ya halmashauri kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Hadi kufikia Desemba 2021, halmashauri zilikuwa zimetenga Sh. 35.7 bilioni kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

### MKAKATI KUONGEZA TIJA

Katika kuhakikisha mikopo hiyo inaongeza tija na kuwakomboa wananchi kwenye umasikini, serikali imeahidi kuongeza usimamizi kwenye matumizi ya mikopo hiyo kwa makundi husika.

Ni hatua inayokuja kutokana na kubainika kuwepo kwa baadhi ya wanufaika ambao, wameshindwa kuzitumia fedha hizo kwenye malengo yaliyokusudiwa na wengine hata kuhama maeneo ikiwemo kutofanyika kwa uhakika wa kutosha.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), taarifa yake inaonyesha kuwepo vikundi vya wanufaika katika mamlaka 185 za serikali za mitaa, ambazo hawakurejesha kiasi cha Sh. 47.01 bilioni walizopewa mikopo.

### HATUA MPYA

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), Innocent Bashungwa, anasema kuanzia sasa serikali itaimarisha usimamizi wa utoaji mikopo ya asilimia 10 kwenye halmashauri, kwa kutumia mifumo ya Tehama.

Ni hatua inayolenga kuwanufaisha wahusika na kuleta mabadiliko chanya kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Bashungwa anasema, mfumo huo wa kielektroniki utasaidia kuongeza usimamizi kwa kutambua anayepewa mkopo, shughuli anayoifanya na urejeshaji wa mkopo husika katika halmashauri zote nchini.

Waziri anafafanua, kuwa miongoni mwa vigezo vinavyotumika kupima ufanisi wa wakurugenzi katika halmashauri ni usimamizi wa utoaji na urejeshaji wa mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

### AJIRA NA UJUZI

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, serikali ilichukua hatua za utekelezaji miradi ya kielelezo, ujenzi wa viwanda, sambamba na kuimarisha sekta binafsi. Ili kuongeza fursa za ajira na ujuzi kwa Watanzania, ikizalisha idadi ya ajira (kujiajiri na kuajiriwa) 584,333.

Pia, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya utafiti wa hali ya nguvukazi nchini kupata viashiria muhimu vitakavyotumika katika kuhuisha, kutunga, kufuatilia na kutathmini sera, mikakati na programu za soko la ajira nchini.

Utafiti huo umeonyesha kiwango cha ukosefu wa ajira nchini kimepungua kutoka asilimia 10.3 mwaka 2014 hadi asilimia 9.0 mwaka 2021, hatua ambayo imeifanya Serikali kuendelea kupunguza makali ya wasio na ajira hasa vijana.

Aidha, nguvukazi ya vijana ni watu milioni 14.2 sawa na asilimia 55 ya nguvukazi yote nchini. Vijana milioni 12.5 sawa na asilimia 87.8 ya nguvukazi ya vijana wameajiriwa au kujiajiri. Sekta ya kilimo imeendelea kuongoza kwa kutoa zaidi ya asilimia 63 ya ajira kwa vijana.

Kupitia utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi, vijana 22,899 wamepatiwa ujuzi unaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Kati ya hao, vijana 14,440 wakiwemo vijana wenye ulemavu 349 wamepatiwa mafunzo ya uanagenzi katika fani za ufundi stadi katika vyuo na taasisi 72 nchini.

Vijana 3,600 wamewezeshwa kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba na vijana 2,644 wamepewa mafunzo ya kurasimishiwa ujuzi walioupata kupitia mfumo usio rasmi.

Pia, serikali imewezesha wahitimu 2,215 kupata mafunzo ya uzoefu kazini katika taasisi binafsi na umma.

Mkakati wa sasa katika mwaka mpya wa fedha 2022/2023, ni kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kutathmini masuala yanayolenga kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kunufaika na fursa zilizopo.

### NENO LA WADAU

Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, anasema jiji hilo linakusanya mapato kadri linavyoweza na kusisitiza ukusanyaji wa kodi ili fedha hizo ziweze kusaidia vikundi hivyo.

"Tunatoa mikopo, mahususi kwa ajili ya vijana, wanawake na wenye ulemavu; mikopo hiyo ni ya vikundi vilivyotaka kununua pikipiki na baiskeli za matatu," Kumbilamoto anasema.

Mkuu wa Ustawi wa Jamii na Vijana Manispaa ya Ilala, Francisca Makoye, anafafanua kuwa uamuzi wa ndani ulifikiwa kuwa kati ya asilimia 10, iliyoagizwa na kanuni ya taifa, vikundi vya wanawake vitapata asilimia 4, vikundi vya vijana (4%) na vya watu wenye ulemavu (2%), mikopo bila riba.





# Gwajima awageukia wanahabari kuhamasisha malezi ya watoto

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, amevitaka vyombo vya habari nchini kuandika habari za malezi ya watoto ili kupunguza vitendo vya ukatili.

Dk. Gwajima alitoa rai hiyo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya kitaifa ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya mtoto kwa waandishi wa habari, yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Aga Khan, TECDEN na CIC wakishirikisha Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

"Hali mbaya ya ukatili iliyopo sasa haiwezi kwisha badala yake watu wataona kuwa ni jambo la kawaida kama kalamu zenu hamtazitumia vizuri kuelimisha jamii kuhusu masuala ya malezi,"alisema. Waziri huyo alisema kwa sasa ukatili kwa watoto ni mkubwa na unachangiwa na mambo mengi.

"Ni wakati wa kufanya mapinduzi makubwa katika habari na kuyafikia makundi mengine kwa kutumia mbinu mbadala ambazo awali hazikuwapo, tunatamani kuona habari za kukemea na kutoa elimu," alisema.

Naye Mwakilishi wa Chuo Kikuu cha Aga Khan, Joyce Malangu, alisema mpango huo ni mkakati wa kujenga jamii bora inayoanzia utotoni.

"Aga Khan imeingia ubia kwenye mpango huu na hasa ukilenga mafunzo ili kupata watu bora watakaokuwa na uwezo mkubwa wa kuandika habari zenye kuibua hisia na mafanikio," alisema.

Mkurugenzi wa CIC, Craing Ferla, alisema mpango wa kusaidia malezi na makuzi ya mtoto tangu siku ya kwanza, umeonekana kufanya vizuri kwa Tanzania kuliko nchi zingine zote za kusini mwa jangwa la Sahara.

Alisema mpango huo ulianza 2019 ambao hadi juzi tayari makala na habari zaidi ya 1450 zinazohusu malezi na makuzi ya mtoto zilishachapishwa.




Makamu wa Rais wa Kampuni ya AngloGold Ashanti anayeshughulikia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo, akipokea tuzo ya kutambua mchango wa kampuni hiyo katika masuala ya afya kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan. Shayo alikabidhiwa tuzo hiyo kwenye uzinduzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya CCBRT mkoani Dar es Salaam. AngloGold Ashanti kupitia Geita Gold Mining Limited ni mmoja wa wadau wa maendeleo wanaounga mkono jitihada za CCBRT kuboresha huduma za afya ya uzazi na mama wajawazito nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yatamka neno miradi ya maendeleo

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, imekagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Jiji la Dodoma na kutaka ijengwe kwa viwango vinavyotakiwa ili iwe na tija kwa wananchi.

Miongoni mwa miradi iliyotembelewa ni pamoja na ujenzi wa madarasa ya fedha za Maendeleo ya Ustawi na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, shule ya sekondari viwandani, ujenzi wa Kituo cha Afya Chang'ombe unaotekelezwa kwa fedha za tozo za miamala ya simu.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa chama hicho mkoani hapa, Damas Mukasa, alipongeza Jiji kwa utekelezaji wa miradi hiyo na kudai kuwa dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona inatekelezwa kwa viwango stahiki na kuwa na tija kwa jamii.

Alisema Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa CCM katika serikali anayoiongoza amekuwa akitoa fedha nyingi kutekeleza miradi ya maendeleo ili kusogeza huduma za msingi kwa wananchi.

Mapema, akitoa taarifa ya miradi mbalimbali, Mkurugenzi wa Jiji, Joseph Mafuru, alisema Oktoba, 2021 Shule ya Sekondari Viwandani ilipokea Sh. milioni 40 za UVIKO-19 ili kujenga madarasa mawili na tayari yameanza kutumika.

Kuhusu Kituo cha Afya Chang'ombe, Mafuru alisema utekelezaji wake unatokana na tozo ambapo Sh. milioni 500 zimepokewa ili kujenga majengo ya mama na mtoto, chumba cha upasuaji, jengo la kufulia na kinatarajia kuanza kutoa huduma mwezi huu baada ya kukamilika manunuzi ya vifaa tiba na samani.

"Mradi utakapokamilika utasaidia watu 30,024 na utapunguza wajawazito kutembea umbali mrefu kupata huduma za kujifungua, lakini utasogeza huduma za kliniki," alisema.

Kuhusu ujenzi wa Kituo cha Afya Nkuhungu, alisema umetekelezwa kwa kutumia vyanzo vya mapato vya ndani. Alisema Sh. milioni 207.9 zimetolewa kujenga majengo ya wagonjwa wa nje na maabara na utasaidia jamii ya watu 38,622.

Kadhalika, alisema ujenzi wa Shule ya Sekondari Hombolo Makulu, unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu na unatekelezwa kwa ufadhili wa Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari(SEQUIP) kwa gharama ya Sh. milioni 600.

Alisema shule hiyo itasaidia wanafunzi kuondokana na adha ya kutembea umbali wa kilometa tisa kufuata shule nyingine ya sekondari.

"Tunaahidi kusimamia kwa umakini matumizi ya fedha hizi na kutekeleza miradi yenye tija ili malengo yaweze kufikiwa na wananchi wapate huduma bora,"alisema.

# TGNP yapanua wigo utetezi wa haki

**Na Peter Mkwavila,**
KONDOA

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TNGP), umefungua kituo cha kusaidia kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa wananchi wa Kijiji cha Haubi, kilichoko katika wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma.

Kituo hicho kinalenga kutokomeza ukatili na kuleta usawa katika upatikanaji wa huduma za kijamii.

Akizungumza katika ufunguzi wa kituo hicho, Ofisa kutoka TGNP, Annagrece Rombiza, alisema mtandao huo umebaini kuwapo kwa vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa miongoni mwa jamii, hivyo kuwapo kwa kituo hicho itasaidia kuondokana na tatizo hilo.

"Bado kuna ukatili unaofanyika kwenye maeneo ya kupata huduma kama vile umiliki wa mashamba, na kwenye upande wa mila na desturi mwanamke kumfanya kiumbe dhaifu na kuishia kuozeshwa licha ya kuwa wadogo," alisema.

Alisema kituo hicho kitasaidia kuleta usawa na kuibua ukatili wa kijinsia ambao unaofanywa miongoni mwa wana jamii.

Rombiza aliwataka wakazi wa kijiji hicho kushiriki katika mikutano ili kutoa kero zao badala ya kuishia kulalamika.

Nao wakazi wa eneo hilo, walipongeza kufunguliwa kwa kituo hicho na kwamba kitakuwa msaada kwa upande wao kwa kuibuliwa kero mbalimbali hususan ukatili wa kijinsia.

Mkazi wa Kijiji hicho, Athumani Rashidi, alisema elimu ya watakayoipata itasaidia utambuzi na kupata huduma sawa za kijamii kama vile kwenye umiliki wa ardhi.

Naye Mariam Hamisi, alisema: "Kituo hiki kitatusaidia kupata elimu dhidi ya ukatili wa kijinsia na jamii sasa itaweza kufahamu vyema aina zote za ukatili wa kijinsia na sasa wataweza kukabiliana nazo pindi vitendo hivyo vinapotokea."

**Rombiza aliwataka wakazi wa kijiji hicho kushiriki katika mikutano ili kutoa kero zao badala ya kuishia kulalamika.**





# Ma-DC na Ma- DED kupongezwa kuvuka lengo ukusanyaji mapato

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOA wa Mbeya umesema unaandaa hafla maalumu ya kuwapongeza wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na wakuu wa idara za fedha za halmashauri kutokana na kufikisha asilimia 105.6 ya ukusanyaji wa mapato ya ndani katika mwaka wa fedha 2021/22.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi alipokuwa anatoa taarifa ya ukusanyaji wa mapato katika mkoa. Alisema walipangiwa kukusanya Sh. bilioni 42.68 lakini wamekusanya Sh.bilioni 45.06.

Alisema makusanyo hayo yalifikiwa kutokana na weledi katika usimamizi uliofanywa na watendaji wa ofisi ya mkuu wa mkoa, wakurugenzi, wakuu wa wilaya na wakuu wa idara katika halmashauri na kwamba ili kuwatia moyo, anakusudia kuwaandalia hafla ya kuwapongeza.

Viongozi hao, alisema watapatiwa vyeti maalumu vya kuwapongeza pamoja na kujumuika nao kwenye eneo mojawapo la vivutio vya utalii ndani ya mkoa ili iwe sehemu ya kuunga mkono filamu ya The Royal Tour iliyoigizwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Tutaenda tujumuike pamoja katika fukwe za Matema zilizoko ndani ya Ziwa Nyasa, viongozi hawa wameonyesha uzalendo wa hali ya juu kwenye makusanyo ya mapato ya ndani," alisema Homera.

Alisema wanakusudia pia kuweka mpango mzuri wa usimamizi wa mapato hayo ili kuhakikisha fedha hizo zilizokusanywa zinatumika vizuri kwenye utekelezaji wa miradi na kuzuia kila aina ya ufisadi.

Homera alisema kati ya halmashauri zote saba za mkoa huo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ndiyo kinara wa ukusanyaji kwa kuwa ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 4.3 lakini imekusanya Sh. bilioni 5.2 sawa na asilimia 121.

Alisema halmashauri ya pili ni ya wilaya ya Chunya ambayo ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 4.8 lakini imekusanya Sh. bilioni 5.2 sawa na asilimia 108.8 ikifuatiwa na Halmashauri ya Busokelo ambayo ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 1.5 lakini imekusanya Sh. bilioni 1.6 sawa na asilimia 104.6.

Halmashauri ya nne ni Jiji la Mbeya ambayo ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 16.6 mpaka kufikia Juni 30, ilikuwa imekusanya Sh. bilioni 17.2 sawa na asilimia 103.7 ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambayo ilitakiwa kukusanya Sh. bilioni 5.3 lakini ikakusanya Sh. bilioni 5.4 sawa na asilimia 103.1.

Homera alisema halmashauri ya sita ni Mbarali ambayo ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 6.07 lakini imekusanya Sh. bilioni 6.2 sawa na asilimia 102.3 na halmashauri ya mwisho ni Kyela ambayo ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 3.8 lakini imekusanya Sh. bilioni 3.9 sawa na asilimia 101.2.

Hata hivyo, Homera alisema mbali na halmashauri hizo kufanya vizuri kwenye ukusanyaji wa mapato, pia taasisi mbalimbali za umma zimefanya vizuri na kwamba wanaendelea kukusanya taarifa ili nazo ziwekwe wazi.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye, baada ya kuwasili katika Shule ya Msingi Iganjo, jijini Mbeya jana, kwa ajili ya kutembelea mradi wa ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo uliofadhiliwa na TEA. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara chuma chakavu waiomba serikali kupunguza tozo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKUSANYAJI na wanunuzi wa vyuma chakavu katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameiomba serikali kuwapunguzia utitiri wa tozo na vibali vya kusafirishia vyuma hivyo kwa madai kuwa kazi yao ni sehemu ya utunzaji wa mazingira.

Pia wamesema utitiri wa tozo hizo na vibali unasababisha biashara zao kushindwa kuendelea kwa kuwa mitaji yao ni midogo, hivyo baadhi yao wanashindwa kuhimili wingi huo wa tozo na vibali.

Walitoa kilio hicho juzi wakati wa mafunzo maalumu yaliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) yaliyokuwa yanalenga kuwaelimisha kuhusu Sheria ya Usafirishaji wa Vyuma Chakavu na Taka Hatarishi.

Mafunzo hayo yaliwahusisha wakusanyaji, wauzaji na wanunuzi wa vyuma chakavu kutoka katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe pamoja na maofisa wa forodha wa mipaka ya Kasumulu na Tunduma.

Mmoja wa wauzaji hao, Alex Swila, alisema biashara yao haitofautiani na wajasiriamali wadogo maarufu kwa jina la machinga lakini tozo wanazotozwa ni kubwa na haziendani na biashara wanayofanya.

Alisema miaka ya nyuma tozo hizo zilikuwa rafiki kiasi kwamba wafanyabiashara wote walikuwa wana hiari kulipa tofauti na sasa ambapo baadhi ya wafanyabiashara wanaamua kuachana nayo kutokana na tozo.

"Vibali ambavyo tunatakiwa kuwa navyo ambavyo vinatolewa na NEMC havipungui vitatu. Sasa mimi mtaji wangu hauzidi Sh. 2,000,000 lakini nikitaka kuwa na vibali vyote nitatakiwa kulipa Sh. milioni 15 jambo ambalo haliwezekani kwangu," alisema Swila.

Alisema wafanyabiashara wengi wanakwepa kulipa tozo hizo kutokana na kutokuwa rafiki, hivyo akaiomba serikali kupunguza gharama ili fedha nyingi zikusanywe na usafi wa mazingira ufanyike. Naye Issa Mwaisabila alisema vibali wanavyotakiwa kuwa navyo ni vya ukusanyaji wa vyuma, kuhifadhia vyuma na kusafirishia na kwamba kama inawezekana serikali ingeviunganisha ili kiwe kimoja.

Alisema ili kuifanya biashara hiyo kuwa rafiki, inatakiwa serikali iwaandalie kibali kimoja kama ilivyo kwa leseni za biashara na kwamba wanatakiwa waendelee kupatiwa mafunzo ya usalama wa biashara hiyo.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira wa NEMC, Mhandisi Redempta Samwel, alisema vyuma chakavu na taka za kielektroniki zina athari za kimazingira na kwamba ndiyo sababu ya kuwekewa sheria.

Alisema taka hizo zimewekwa kwenye kundi la taka hatarishi na kwamba zipo sheria mbalimbali za usimamizi wa taka hizo zikiwamo sheria za kimataifa zilizoainishwa kwenye mkataba wa kimataifa wa mazingira.

"Moja kati ya kanuni za usimamizi wa taka hizi hatarishi ni ya mwaka 2009, baadhi ya taka hizi zimeibua fursa kwa vijana hasa zile ambazo zinatumika kama malighafi kwenye viwanda na hivyo tumeona ni vema tutoe mafunzo haya kwa hawa wadau," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alishauri NEMC kutunga sheria ndogo za kuwatambua na kuwadhibiti wakusanyaji wa vyuma hivyo ili kuepuka kutumia fursa hiyo kuharibu miundombinu.

# Mbaroni tuhuma za wizi wa magari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU sita wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kutokana na tuhuma mbalimbali zikiwamo za wizi wa magari na pikipiki katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, aliyasema hayo jana alipozungumza na wandishi wa habari kuhusu oparesheni mbalimbali zilizofanywa na jeshi hilo katika maeneo mbalimbali ya mkoa.

Alisema katika tukio la kwanza, waliwakamata watuhumiwa watatu wa wizi wa magari na pikipiki ambao pia walikutwa na baadhi ya vyombo hivyo vya wizi.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Yusuph Ramadhan (26) mkazi wa Ferest na Abuu Lutangalama (26) mkazi wa Itezi jijini Mbeya pamoja na Shukuru Nyema (23) mkazi wa Songea mkoani Ruvuma.

"Jeshi la Polisi tulifanya upekuzi wa kisheria na tuliwakuta wahusika na magari manne ambayo walikiri ni ya wizi, magari hayo ni Toyota IST matatu yenye namba za usajili T.786 DLD na T.649 DMH na moja ambalo halina namba pamoja na Toyota Spacio isiyo na namba za usajili," alisema Matei.

Alisema watuhumiwa baada ya kuhojiwa walikiri pia kuhusika na matukio mbalimbali ya wizi wa magari katika mikoa ya Dar es Salaam na Njombe kwa nyakati tofauti.

Katika tukio linguine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia watu watatu kwa kosa la kukutwa na nyara za Serikali ambazo ni meno ya Tembo .

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Rashid Mwajanga (33) mkazi wa Lupa wilayani Chunya, Juma Mtenga (42) mkazi wa Mbuyuni wilayani Songwe na Cosmas Ranwelu (25) mkazi wa Lupa wilayani Chunya.

Alisema watuhumiwa hao walikutwa na vipande 10 vya meno ohayo vyenye uzito wa Kilogramu 7.1 ambavyo vinakadiriwa kuwa na thamani ya Sh. milioni 69.47 na kwamba ni sawa na tembo wawili waliouawa.

Alisema upelelezi wa matukio yote mawili unaendele na kwamba ukikamilika wahusika watafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria na akawataka wananchi kuhakikisha wanafanya shughuli halali za kujiingizia kipato.



## Mpango wa kufufua karafuu sasa waiva

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Othman Masoud Othman, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inakusudia kufufua kilimo cha mikarafuu ili kufikia uzalishaji wa kati ya tani 15,000 hadi 20,000 kwa mwaka.

Othman aliyasema hayo jana ofisini kwake, Migombani mjini Zanzibar alipofanya mazungumzo na Balozi wa Tanzania nchi Indonesia, Makocha Moshe Tembele, aliyefika kumuaga kwenda katika kituo chake cha kazi baada ya kuteuliwa hivi karibuni katika wadhifa huo.

Alisema hivi sasa uzalishaji wa karafuu Zanzibar umeshuka na kwamba msimu mkubwa mavuno yanayopatikana ni wastani wa tani 8,000 kiasi ambacho ni kidogo katika kusaidia juhudi za kukuza uchumi wa wananchi na Zanzibar kwa jumla.

Othman alisema kutokana na hali hiyo, serikali imeona kuna umuhimu mkubwa wa kukifufua kilimo hicho ili kuwa na tija zaidi kiuchumi kwa Zanzibar, hivyo kumtaka balozi huyo kutumia fursa ya uzoefu na utaalamu wa Indonesia kusaidia kuiwezesha nchi kupata maarifa zaidi ya uendelezaji wa karafuu.

Kuhusu biashara, Othman alisama kuna umuhimu wa kutoka katika uzalishaji pekee wa zao hilo na kuingia katika hatua ya usarifu kwa lengo la kulifanya kuwa na manufaa zaidi kwa wananchi na taifa kwa jumla.

Alisema Indonesia inazo fursa nyingi za kibiashara na kumtaka Balozi Tembele kusaidia kuzitangaza na wananchi na wafanyabiashara Zanzibar kuzitumia ili kufaidika nazo katika jitihada za kukuza uchumi na maendeleo ya nchi.

Pia alimtaka kusaidia kutenegeneza mazingira bora ya kuwasaidia wafanyabiashara wa Tanzania ikiwamo kushajiisha uwekezaji wa ushirikiano kati ya Watanzania na wafanyabiashara wa Indonesia.

Naye Balozi Tembele aliahidi kwamba atajitahidi kuzitumia vyema fursa za kiuchumi na kibiashara zilizoko Indonesia ili kutumika vyema kuwafaidisha Watanzania.

# Waliowekewa betri washukuru SMZ

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAGONJWA waliopatiwa matibabu ya kuwekewa betri za mapigo ya moyo katika Hospitali ya Mnazimmoja, wameipongeza serikali ya Zanzibar kuwapatia huduma hiyo bure.

Wakizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar, walisema matibabu hayo waliyopatiwa bila kutozwa gharama yoyote, yamewapatia nafuu kiafya.

Alisema serikali imeonyesha kuwathamini wananchi wake na ni ukweli kwamba matibabu hayo ni gharama na wananchi wengi hali zao za maisha ni duni.

Mmoja wa wagonjwa hao, Masika Apata Mwalim (58) mkazi wa Kwahani mjini Unguja, aliishukuru serikali kwa kumsaidia tiba hiyo ambayo hivi sasa afya yake inaendelea vizuri.

Alisema amehangaika kutafuta tiba ya maradhi hayo kwa kipindi cha miaka miwili lakini kwa sasa anashukuru kupata matibabu hayo ambayo yamemsaidia kupata unafuu.

"Hospitali zote za Zanzibar unazozijua mimi nimehangaika na nimefika mpaka hospitali ya Muhimbili. Nilikuwa naumwa sijifahamu, sili, nikila natapika.

Hata nikitembea nanguka na napoteza fahamu lakini hivi sasa nashukuru tokea kupatiwa matibabu haya naishukuru serikali imenisaidia sana," alisema.

Alisema hivi sasa anashukuru anakula vizuri lakini amekuwa akifuata miiko kwa kupunguza mafuta na chumvi na kumpongeza daktari bingwa wa magonjwa hayo kwa kufuatilia kujua maendeleo yao.

Naye Jabu Ali (72) mkazi wa Jang'ombe, alisema tangu amefanyiwa matibabu hayo amepata nafuu.

"Kama si serikali kutusaidia kutupatia matibabu haya, hivi sasa ningekuwa na hali mbaya. Ningepata wapi Sh. milioni 10 kwa ajili ya matibabu?" Alisema.

Pia aliwashauri wananchi kuchunguza afya zao ili kujua matatizo yanayowakabili na kupatiwa matibabu mapema na kuacha kutumia vyakula vya mafuta ili kujiepusha na magonjwa.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Khamis Mustafa Khamis, alisema hospitali hiyo kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa Norway, imefanikiwa kwa mara ya kwanza Zanzibar kuwawekea betri wagonjwa watano wakiwamo wanawake wawili na wanaume watatu wenye maradhi ya mfumo duni wa umeme.

Alisema wagonjwa wote kwa sasa wanaendelea vizuri na kazi hiyo itakuwa endelevu na Novemba, mwaka huu, wanatarajia kufanya matibabu kama hayo kwa wagonjwa ambao wana matatizo ya mfumo wa umeme na mapigo ya moyo.

Alisema betri hizo zimewekewa uwezo wa miaka 10 na inapomalizika chaji zinabadilishwa na kuwawekea zingine.




Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji (wapili kulia), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (wapili kushoto), alipotembelea maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Latifa Mohamed Hamis. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasisitizwa kutoa huduma upatikanaji haki kwa wakati

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WASAIDIZI wa sheria wamesisitizwa kusaidia upatikanaji wa huduma stahiki kwa waathirika wa matukio ya udhalilishaji katika maeneo yao.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, aliyasema hayo juzi katika mkutano wa kutathmini utekelezaji wa mipango kazi ya vikundi vya wasaidizi wa sheria vya wilaya katika kupambana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema pamoja na kuwapo kwa muamko mkubwa kwa wananchi kuripoti matukio hayo ya udhalilishaji, bado waathirika wengi hawafahamu mahali pa kwenda wanapopatwa na majanga hayo.

Naibu Waziri alisema ni vyema kwa wasaidizi hao kuongeza bidii katika utekelezaji wa majukumu yao na kushirikiana ili kuhakikisha lengo la serikali la kupambana na matukio hayo linafikiwa.

Alisema kwamba serikali inachukua jitihada mbalimbali ikiwamo kubadilisha sheria kuondosha dhamana kwa watuhumiwa ili kuona inapambana na matendo hayo ambayo yakipoteza nguvu kazi ya taifa.

Mkuu wa Division ya Jinsia na Watoto, Halima Abrahman, alisema malengo ya mkutano huo ni kupokea taarifa na utekelezaji wa mipango kazi ya Aprili- Juni 2022 za vikundi vya wasaidizi hao katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia na kubaini changamoto zilizojitokeza katika kupambana na vitendo hivyo.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa wa mpango kazi kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu, Msaidizi wa Sheria kutoka Wilaya ya Kati, Kombo Mohd, alisema shule 12 na madrasa sita zimefikiwa na kupatiwa elimu na wanafunzi 2,812 wakiwamo wasichana 1,720 na wavulana 1,092 walipatiwa elimu hiyo.

Pia alisema mabaraza ya vijana matano na vikundi vya kinamama vinne na kikundi kimoja cha wavuvi vyenye wanajamii 3,458 wakiwamo wanawake 2,243 na wanaume 1,215 vilipatiwa elimu kuhusu udhalilishaji na masuala mengine.

Alisema kamati imefanya ufatiliaji wa mashauri ya waathirika kwenye madawati ya jinsia na ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ambapo mashauri 35 ya zamani na mapya yalifanyiwa ufuatiliaji na kwamba mashauri 11 yamekamilika na 24 yako kwenye hatua.

Nao wasaidizi wa sheria, walisema kuna mwamko katika jamii wanapoitisha mikutano umekuwa mdogo na kukosa ushirikiano wa upatikanaji wa taarifa kamili katika idara husika.

# MAONYESHO YA 46 YA BIASHARA YA KIMATAIFA



Katibu Mkuu Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AFCFTA), Wamkele Mene (wa tatu kushoto), akimsikiliza Mtafiti wa Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Jacqueline Mwendwa (kushoto), akitoa ufafanuzi wa kuongeza thamani kwenye maganda ya chungwa kwa kuzalisha mafuta tete yanayotumika kama malighafi viwandani kuzalisha losheni na vitu mbalimbali, katika maonyesho hayo. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Ofisa Mwandamizi wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) Kitengo cha Maendeleo ya Biashara, Eunice Michael Msangi (kushoto), akitoa elimu kwa baadhi ya wananchi waliotembelea banda la Maliasili na Utalii, katika maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam 'Sabasaba', jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), James Mataragio (kulia), akizungumza na waandishi wa habari katika banda la shirika hilo katika maonyesho hayo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mkurugenzi wa Tume ya Ushindani (FCC), William Erio (kulia), akimsikiliza Naibu Waziri Uwekezaji Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alipotembelea maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), akimhudumia mteja katika banda la benki hiyo, wakati wa maonyesho hayo. Benki hiyo imetumia maonyesho hayo kutoa huduma pamoja na elimu ya fedha kwa makundi mbalimbali. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## HABARI KIMATAIFA

# Russia yakaribia kuikamata Sloviansk

**Kyiv,** UKRAINE

SHUGHULI ya uokoaji wa raia kutoka eneo la Sloviansk nchini Ukraine, inaendelea wakati vikosi vya Russia vinazidi kukaribia mji huo.

Vikosi vya Russia vinazidisha kampeni yao ya kuuteka ili kupata udhibiti kamili wa eneo la Donbas. Vita kati ya nchi hizo mbili inatimia siku ya 134 tangu Russia kuvamia Ukraine.

Hata hivyo, mji wa Sloviansk umekuwa ukikabiliwa na mashambulizi makali siku tatu mfululizo.

Waandishi wa habari wa shirika la habari la Ufaransa (AFP) walisema wameona maroketi yakianguka katika soko la Sloviansk na mitaa ya karibu huku maofisa wa zimamoto wakipambana kuzima moto.

**Mashambulizi ya makombora ya Russia yameteketeza soko kuu katika mji wa Sloyansk mashariki mwa**

Karibu theluthi moja ya soko hilo linadaiwa kuharibiwa na sehemu iliyosalia inaendelea na shughuli zake huku wateja wakionekana kununua matunda na mboga mboga.

Meya wa mji huo Vadym Lyakh, alisema karibu watu 23,000 kati ya 110,000, bado wamesalia Sloviansk, ila akadai Russia imeshindwa kuuzingira mji huo. Donbas mashariki inajumuisha eneo la Luhansk ambalo tayari limetekwa na Russia na Donetsk ambalo ndilo eneo linalolengwa sasa hivi.

**SRI LANKA YAIOMBA RUSSIA KUNUNUA MAFUTA**

Rais wa Sri Lanka, Gotabaya Rajapaksa amesema amemwomba kiongozi wa Russia, Vladimir Putin kulisaidia taifa lake lenye matatizo ya fedha kuagiza mafuta wakati huu ambao nchi yake inakabiliwa na mzozo mkubwa zaidi wa kiuchumi tangu ilipopata uhuru wake kutoka kwa Uingereza mwaka 1948.

Alisema alikuwa na mazungumzo yenye tija na Putin.

"Niliomba msaada wa mkopo kuagiza mafuta," Rajapaksa alitwiti akimaanisha mazungumzo yake na kiongozi huyo wa Russia.

Hii inakuja baada ya waziri wa nishati wa Sri Lanka kuonya mwishoni mwa juma kwamba nchi hiyo huenda ikakosa petroli hivi karibuni.

Russia inayoshika nafasi ya tatu kwa uzalishaji mafuta, imetangaza kuuza kwa bei nafuu kutokana na vikwazo vilivyowekwa na nchi za Magharibi vya kupunguza ununuzi wa nishati ya mafuta na gesi.

Rajapaksa pia alisema ameomba kwa unyenyekevu safari za ndege kutoka nchini mwake hadi Russia kuanza tena baada ya shirika la ndege la Aeroflot kusimamisha huduma mwezi uliopita. **DW**

## Hatimaye Boris Johnson ajiuzulu

**LONDON,** Uingereza

BAADA ya kupata shinikizo kubwa kutoka kwa wabunge wa chama chake, hatimaye Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson, amejiuzulu wadhifa wake.

Akitoa hotuba yake ya kujiuzulu jana, Johnson alisema anasikitika kuacha kazi hiyo ambayo aliitaja kuwa nzuri zaidi duniani.

"Ninasikitika kuacha kazi nzuri zaidi duniani lakini ndiyo hali halisi.Ninataka ujue jinsi ninavyohuzunishwa na kuacha kazi bora zaidi duniani," alisema Johnson.

Aliongeza "Nimekubaliana na Sir Graham Brady, mwenyekiti wa wabunge wetu wa viti maalum, kwamba mchakato wa kumchagua kiongozi mpya uanze sasa na ratiba itatangazwa wiki ijayo,"

Hata hivyo akasisitiza "Na leo (jana) nimeteua Baraza la Mawaziri kuhudumu, pia nitaendelea kuongoza hadi kiongozi mpya atakapochaguliwa." Aidha, alisema jinsi anavyohuzunishwa kuona miradi aliyoanzisha anaiacha.

"Inatia uchungu kutoona miradi yangu ikikamilika" alisema.

Hata hivyo, Johnson alisema ni jambo la upuuzi kubadilisha serikali na kukataa wazo la uchaguzi mkuu wakati wanatimiza majukumu mengi na makubwa wakati hali ya kiuchumi ikiwa ngumu ndani ya nchi na kimataifa.

"Najuta kutofanikiwa katika majadiliano na inatia uchungu kutoona mawazo na miradi mingi ikitimia."

Johnson alishukuru umma kwa kumpa upendeleo mkubwa wakati akitimiza wajibu wake.

Alisema utaendelea kuhudumia hadi waziri mkuu mpya atakapochukua wadhifa huo. Waziri mkuu amemaliza kauli yake kwa kusema kwamba hadi pale atakapopatikana mbadala wake, maslahi ya umma yaendelee kutekelezwa.

"Kuwa waziri mkuu ni elimu ya kipekee nimesafiri kila sehemu ya Uingereza na nimekutana na watu wengi wenye asili ya Uingereza, wako tayari kushughulikia matatizo ya zamani kwa njia mpya." Alimalizia kusema katika hotuba yake. **BBC**



Waumini wa Kiislamu wakiwa kwenye ibada ya Hija iliyoanza jana. **PICHA: BBC**

## Waislamu milioni moja waanza Hijja

**MAKKA,** Saudia Arabia

IBADA ya Hijja kwa waumini wa dini ya kiislamu imeanza rasmi jana katika mji mtakatifu wa Makka nchini Saudi Arabia.

Maelfu ya waumini wamekusanyika katika mji huo wakitokea nchi mbali mbali duniani. Ibada ya Hajj ni nguzo ya mwisho katika nguzo tano za imani ya kiislamu na ni ibada inayohimizwa kufanywa na kila muumini aliyekuwa katika uwezo wa kiafya na kiuchumi.

Ibada hiyo inafanyika tangu lilipozuka janga la virusi vya Corona miaka mitatu iliyopita, na ndiyo ibada inayofanywa na watu wengi tangu Saudi Arabia kutangaza kuruhusu mahujaji milioni moja kushiriki.

Mwaka 2020 na 2021 Saudi Arabia ilizuia raia kutoka nchi za kigeni kushiriki ibada hiyo kutokana na mlipuko wa janga la Corona lililopiga duniani.

Mohammed ni raia wa Uingereza mwenye asili ya Iraq,yeye aliamua kutembea zaidi ya kilomita 7,000 kwa miguu akisukuma kigari alichotia vitu vyake vya matumizi kutoka Uingereza akipitia nchi tisa kabla ya kuvuka kutoka Jordan na kuingia Saudi Arabia katika mji wa Tabuk kaskazini magharibi. **DW**

## DRC, Rwanda wakubali kusitisha mapigano

**LUANDA,** Angola

VIONGOZI wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Rwanda wamekubaliana kuwa na mpango wa kupunguza mapigano.

Hatua hiyo inatokana na wiki kadhaa kuongezeka kwa mivutano kuhusiana na kikundi cha waasi wa M23 mashariki mwa DRC.

Taarifa hiyo ilitolewa na Ofisi ya rais wa DRC, baada ya mazungumzo ya upatanishi yaliyofanyika nchini Angola.

Mpatanishi wa mazungumzo hayo, Rais Joao Laurenco, amekwenda hatua moja zaidi kwa kutangaza kwamba nchi hizo mbili zimekubaliana kusitisha kabisa mapigano, ila hakutoa taarifa zaidi kuhusiana maafikiano hayo.

Rais Laurenco aliyasema hayo baada ya mkutano uliohudhuriwa na Rais wa Rwanda, Paul Kagame na mwenzake wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Felix Tshisekedi katika Mji Mkuu wa Angola, Luanda.

Kumekuwa na mapigano kati ya jeshi la DRC na waasi wa M23 kwa wiki kadhaa.

Hata hivyo, DRC inaituhumu Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi hao, madai ambayo Rwanda inakanusha. **BBC**

## HABARI MICHEZO

# GOFU WANAWAKE AFRIKA YAHITAJI SH. MILIONI 600

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), kimesema kinahitaji Sh. milioni 600 ili kufanikisha mashindano ya mchezo huo ya wanawake ya Afrika (All African Challenge Trophy), yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Septemba 3 hadi 13, mwaka huu kwenye viwanja wa Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Rais wa TLGU, Sophia Viggo, alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kugharamia zawadi za washindi, chakula na malazi ya washiriki kwa muda wote wa mashindano.

Viggo alisema shindano hilo litashirikisha wachezaji 200 kutoka mataifa 24 ambayo yamethibitisha kuleta nyota wake katika michuano hiyo.

**"Tunaomba tuungwe mkono ili kufanikisha fedha hizo zinapatikana, tutahudumia washiriki wanawake kutoka mataifa mbalimbali hapa barani Afrika ili kufanikisha shindano hili kama ili vyopangwa," alisema Viggo.**

Alisema wachezaji wa timu ya taifa ya Tanzania ambayo itashiriki katika mashindano hayo kwa sasa ipo Kenya ikijiandaa kuchuana katika michuano Open Coast inayotarajiwa kufanyia baadaye mwezi huu kama sehemu ya kujiimarisha kuelekea michuano ya Afrika.

"Mashindano hayo ya Open Coast ni kipimo cha maandalizi ya kujiandaa na mashindano ya Afrika, baada ya timu kutoka Kenya itarejea nchini na kuingia moja kwa moja kambini kwa ajili ya All African Challenge Trophy," alisema kiongozi huyo.

Aliwataja wachezaji wanaounda timu ya Tanzania kuwa ni pamoja na Madina Iddi ambaye ni bingwa anayetetea taji lake la Open Coast, Angel Eaton, Hawa Wanyeche na Neema Olomi.

Naye Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha, alisema baraza hilo ambalo ndio linasimamia dhamana ya michezo watahakikisha wanashirikiana vyema ili kufanikisha shindano hilo linafanikiwa.

"Tanzania tunatarajia kuwa mwenyeji wa mashindano haya ya kimataifa, yanasaidia pia kutangaza utalii wa nchi, tunaunga mkono na kuwaomba wadhamini mbalimbali kujitokeza kuhakikisha fedha hizo zinapatikana kwa ajili ya kutangaza taifa letu," alisema Msitha.

Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa michuano hiyo baada ya viwanja vyake vya Gymkhana kufikia ubora wa kimataifa.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (katikati), akicheza bao na Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani, jijiji Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa. **PICHA: MAELEZO**

# JKU yataka zawadi nono Z'bar

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa JKU FC, inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Sheha Khamis Rashid amelishauri Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) kuzungumza na mdhamini mkuu wa ligi hiyo ili kuongeza kiwango cha zawadi anayopata timu inayoibuka bingwa kwa msimu ujao.

Sheha alisema zawadi kubwa zitasaidia kuongeza ushindani wa ligi na kunyanyua viwango vya wachezaji.

Hata hivyo kocha huyo alipongeza kiasi kilichotolewa katika msimu huu hakikuwa kidogo ikilinganishwa na misimu ya nyuma iliyopita.

"Kusema kweli tumesonga mbele ukilinganisha na tulipotoka, lakini ipo haja ya kuongezwa kiwango hicho ili ilete ushindani zaidi," alisema Sheha.

Alisema kiwango cha Sh. milioni 50 kilichotolewa ni kikubwa lakini anapendekeza kuona timu zote nne zilizomaliza kwenye nafasi ya juu kupata zawadi.

"Ligi ilianza vizuri katika mzunguko wa kwanza lakini hata katika mzunguko wa pili katika michezo ya awali, ila ligi ilikuja kuharibika michezo mitano ya mwisho pale ambapo bingwa alipojulikana hivyo ikakosa ushindani kama wa mwanzo, lakini kama kungekuwa na zawadi kwa timu zinazomaliza nafasi nne za juu, " Sheha alisema.

Aliongeza pia ZFF na Bodi ya Ligi Zanzibar wanatakiwa kukaa na mdhamini huyo kufanyia kazi changamoto mbalimbali zilizotokea katika msimu uliopita ikiwamo kutoa mapema fedha za vilabu ili kusaidia kukamilisha usajili wa wachezaji.

## Zigah asajiliwa Dodoma Jiji FC

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Dodoma Jiji FC, umetangaza rasmi kumalizana na mshambuliaji wa kimataifa kutoka Ghana, Christian Zigah aliyekuwa akiichezea Biashara United ya mkoani Mara ambayo imeshuka daraja, imefahamika.

Zigah ambaye ni mchezaji wa pili kutambulishwa na Dodoma Jiji baada ya juzi kumtambulisha kiungo, Collins Opare, naye pia akitokea Biashara United, amesaini mkataba wa mwaka mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Fortunatus Johnson alisema wamekamilisha usajili wa straika huyo na hiyo imetokana na mahitaji ya benchi la ufundi yenye lengo la kuimarisha kikosi cha msimu ujao.

"Katika usajili huo tutasajili wachezaji 10, wanne kutoka nje ya mipaka ya Tanzania ambao watakuwa ni washambuliaji na winga, lakini nafasi ya kipa tunaangalia mzawa, kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu yetu kuelekea msimu ujao," alisema Fortunatus.

Aliongeza hawatakuwa na mabadiliko katika benchi la ufundi ambalo kwa sasa liko chini ya Kocha Mkuu, Masoud Djuma ambaye amepanga kikosi chake kitaanza mazoezi rasmi ifikapo Julai 15, mwaka huu.

## Polisi Tanzania kusajili wapya 8

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Polisi Tanzania linatarajiwa kukabidhi ripoti yao ya msimu wa Ligi Kuu Bara uliomalizika leo kwa mabosi wa timu hiyo walioko jijini Dodoma huku ikiwekwa wazi wamejipanga kusajili wachezaji wapya nane, imeelezwa.

Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo, aliliambia gazeti hili wanatarajia kukabidhi ripoti hiyo ambayo imeainisha maeneo muhimu wanayohitaji kuyaporesha ili kukiimarisha kikosi chao.

"Kesho (leo) tutakuwa Dodoma kwa ajili ya kukabidhi ripoti yetu ambayo imeonyesha nani na nani tunamhitaji na tusiyemhitaji kwa ajili ya msimu ujao," alisema Mketo.

Kocha huyo alisema wachezaji wapya watakaowasajili watakiongezea nguvu kikosi hicho kwa ajili ya kukabiliana na ushindani wa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara itakayofanyika kuanzia Agosti 17, mwaka huu.

Alitaja nafasi ambazo wamebaini zinamapungufu ni pamoja na ya ushambuliaji, kiungo na ulinzi.

Aliongeza pia wanatarajia mabosi wao watakamilisha mapema mazungumzo na wachezaji ambao mikataba yao imemalizika lakini bado wanahitaji kuendelea nao.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**TIELEMANS KUTUA ARSENAL**

KLABU ya Arsenal ina uhakika wa kuipiku Manchester United kwenye usajili wa pauni milioni 30 wa kiungo wa kati wa Leicester na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25. ***(Sun)***

**ANTONY ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United wametoa dau la pauni milioni 51 kumnunua mshambuliaji wa Ajax, Mbrazil Antony mwenye umri wa miaka 22, lakini klabu hiyo ya Uholanzi inashikilia dau la pauni milioni 68. ***(Goal)***

**NUNES KUTUA CHELSEA**

CHELSEA inaandaa dau la pauni milioni 38 kumnunua kiungo wa kati wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Matheus Nunes, ambaye pia analengwa na Wolves. ***(A Bola)***

**FOREST KUMNASA RICHARDS**

KLABU ya Nottingham Forest inatumaini kukamilisha mikataba ya mlinzi wa kushoto wa Bayern Munich, Omar Richards mwenye umri wa miaka 24, na mlinzi wa kulia wa Liverpool, Neco Williams wa Wales (21), ifikapo wikendi. ***(Athletic)***

**WILLIAMS SOKONI EPL**

KLABU ya Southampton pia wanavutiwa na Neco Williams na wanatumaini kumpiku Nottingham Forest kwenye saini ya beki huyo. ***(Football Insider)***

**GORDON MAMBO SAFI**

KLABU ya Everton inajiandaa kumpa mkataba mpya winga wa Timu ya Taifa ya England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21 ili kuzuia nia ya Newcastle United. ***(Times)***

**EVERTON: LEWIN HAUZWI**

KLABU ya Everton pia haina mpango wa kumuuza mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin na wanaweza kumpa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 mkataba mpya pia. ***(Mirror)***

**RAPHINHA MAMBO BADO**

LEEDS United wamewataka Barcelona kutoa ofa ya mwisho kwa Raphinha wiki hii kwani wanataka mustakabali wa mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Brazil kutatuliwa haraka iwezekanavyo. ***(Sport)***

**MORGAN AGEUKA LULU**

KLABU ya Crystal Palace wana matumaini ya kuzishinda Everton na Nottingham Forest katika kumnasa kiungo wa kati wa Wolves, Morgan Gibbs-White mwenye umri wa miaka 22. ***(Talksport)***

**PALACE, DOWNES WATETA**

CRYSTAL Palace wako kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Swansea, Flynn Downes mwenye umri wa miaka 23, kwa pauni milioni nane. ***(Mail)***

**ARSENAL KUMUUZA PEPE**

ARSENAL wanataka kuuza wachezaji saba - akiwamo winga wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast ambaye alisajiliwa kwa rekodi ya klabu, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 27.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# STERLING ATHIBITISHA KUONDOKA MAN CITY

**Sasa anajiandaa kujiunga na Chelsea baada ya kukamilisha...**

**MANCHESTER,** England

RAHEEM Sterling amekubali makubaliano binafsi na Chelsea baada ya kuthibitisha kwa Manchester City kuwa anataka kuondoka katika klabu hiyo, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mkataba wake unamalizika pale City msimu ujao wa joto, na mabingwa hao wa Ligi Kuu England walikuwa wamemwongezea mkataba.

Lakini 90min ithibitisha Sterling ameiambia klabu hiyo hataki kuongeza mkataba wake na angependa kuondoka msimu huu wa joto.

**City kila mara walimwambia Sterling, kama vile Gabriel Jesus aliyejiunga na Arsenal wiki hii, kwamba wangemuuza msimu huu wa joto ikiwa hatakubaliana na masharti na sasa mabingwa hao wa Ligi Kuu wako tayari kuidhinisha uhamisho wa kwenda Chelsea.**

Sterling alikuwa anafikiria chaguo la kuhamia nje ya nchi kupitia uhamisho wa bure msimu ujao - ambayo ni dhamira iliyothibitishwa anayo, lakini sasa ameamua kuchukua chaguo la kwenda Chelsea.

Thomas Tuchel aliangazia Sterling kama shabaha yake kuu ya ushambuliaji anapotaka kujenga upya safu ya mbele ya klabu - ambapo alianza kwa kumuuza Romelu Lukaku aliyejiunga na Inter Milan.

Kama 90min ilivyofichuliwa mapema wiki hii, City wako tayari kufanya biashara ya takribani pauni milioni 50, huku Chelsea wakiwa tayari kukubaliana na masharti yao.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,012,7

MECHI KALI
LESOTHO
VERSUS
MAURITIUS
1 | 1.64
X | 4.30
2 | 3.86

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# VINICIUS AMPA BALLON D'OR BENZEMA



**MADRID,** Hispania

VINICIUS Junior amesema anakabiliwa na "njia ndefu" kuwania Ballon d'Or, huku akimdokeza mchezaji mwenzake, Karim Benzema anaweza kuwa mchezaji bora wa dunia mwaka huu.

Vinicius alifunga bao pekee kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Real Madrid ikiilaza Liverpool na kushinda taji lao la 14 Mei, akiwa pia na mchango mkubwa katika ushindi wa Los Blancos wa La Liga.

Mbrazil huyo alifunga mabao 22 na kutengeneza asisti 16 katika mashindano yote msimu wa 2021-22.

"Ni (Ballon d'Or) kitu ambacho kinapaswa kuja kwa kawaida," alisema Vinicius alikiambia YouTube Que Papinho.

"Karim ana umri wa miaka 35 na sasa atashinda, Modric alishinda akiwa na miaka 33 (mwaka 2018).

"Nina miaka mingi ya kubadilika, njia ndefu sana kwangu ikiwa Mungu anataka nishinde siku moja."

"Nina umri wa miaka 21 pekee. Nataka kuwafuata wachezaji kama Karim, Modric, Marcelo, ambao walishinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya," aliongeza.



## *Utd kumruhusu Ronaldo kuondoka*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United itamruhusu Cristiano Ronaldo kuondoka Old Trafford msimu huu wa joto na wanatarajia ofa kutoka kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Chelsea.

Uongozi wa United na kocha, Erik ten Hag ulidaiwa kushtushwa wakati Ronaldo na wakala wake, Jorge Mendes walipowaambia mapema mwezi huu angependa kuondoka msimu huu wa joto.

Ten Hag alikuwa akimpanga Ronaldo kuwa kitovu cha mipango yake ya msimu ujao, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 anataka kucheza sehemu nyingine.

Ronaldo alirejea United chini ya mwaka mmoja uliopita akitokea Juventus, na kufunga mabao 24 katika michuano yote katika msimu wake wa kwanza akiwa Old Trafford.

Kushindwa kwa United kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya pia kumeathiri uamuzi wa Ronaldo, United wameweka wazi ataruhusiwa kuondoka licha ya kuwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa.

Inaaminika United watamruhusu Ronaldo kuondoka kwa ada ya wastani ya pauni milioni 15, lakini klabu yoyote itakayomsajili italazimika kumlipa mshahara wake wa zaidi ya pauni 400,000 kwa wiki.

## HABARI MICHEZO



798,111/-

# MAYANGA AAHIDI MTIBWA ITAFANYA USAJILI MKUBWA

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya pili katika misimu miwili mfululizo, Mtibwa Sugar imeponea chupuchupu kushuka daraja baada ya kuiondoa Tanzania Prisons kwa jumla ya mabao 3-2, imeahidi itafanya usajili wa 'kibabe' ili kujiepusha na janga la kufanya vibaya kwenye Ligi Kuu Bara msimu ujao.

**Mtibwa Sugar imesalia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupata ushindi wa ugenini wa mabao 3-1 katika mechi ya kwanza ya 'play off' na juzi ilifungwa goli 1-0 kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.**

Kwa matokeo hayo, Prisons sasa itakutana na JKT Tanzania inayoshiriki Ligi ya Championship, ili kusaka tiketi ya kusalia Ligi Kuu huku maafande wenzao wakitaka kurejea kwenye ligi hiyo ya juu nchini.

Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga alisema walicheza mfumo ule ule ambao waliutumia katika mechi ya kwanza licha ya kwamba walicheza nyumbani, lakini kilichowaathiri wachezaji wake ni uchovu wa safari.

"Tulicheza vilevile kama mechi ya mwanzo, tulikaa nyuma na kushambulia kwa kushtukiza kama tulivyocheza kwao, lakini wachezaji wangu safari hii hawakuwa na kasi kwa sababu ya uchovu wa safari," alisema Mayanga.

Kocha huyo aliwashukuru wachezaji wake na uongozi wa klabu hiyo kwa kufanikisha kubakia kwenye Ligi Kuu, huku akigusia kufanya usajili mkubwa.

"Tutafanya usajili mkubwa, hii mara kwa mara kucheza 'play off' siyo nzuri, tunatakiwa tuboreshe baadhi ya sehemu, kuna maeneo tutayafanyia kazi, kama la ushambuliaji na kiungo. Kusema kweli kuna maeneo mengi tu ya kuyatazama, ni lazima tufanye usajili, nitakaa na viongozi wangu kwa ajili ya kufanikiwa hilo," alisema Mayanga, mchezaji wa zamani wa timu hiyo.

Msimu uliopita pia Mtibwa Sugar ilifanya kama hivi, ilipoichapa Transit Camp mabao 4-1 katika mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam na mechi ya marudiano ikachapwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro, hivyo kubaki kwa matokeo ya jumla ya ushindi wa mabao 4-2.



Wanafunzi wa karate wa Klabu ya Scorpion ya jijini Dar es Salaam wakiwa wamekabidhiwa vyeti maalumu baada ya kuhitimu mafunzo na kukabidhiwa mikanda meusi (black belt) ya mchezo huo. Klabu ya Scorpion iko chini ya Mkufunzi mkongwe, Sensei Jerome Mhagama. **PICHA : MPIGAPICHA WETU**

# Sopu afikiria kucheza Ulaya



**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI mpya wa Azam FC, Abdul Suleiman 'Sopu' amesema lengo lake ni kuona anapata nafasi ya kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya Tanzania.

Sopu amejiunga na Azam FC kwa mkataba wa miaka mitatu akitokea Coastal Union ya jijini Tanga.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Sopu alisema licha ya kupata tuzo ya Mfungaji Bora katika mashindano ya Kombe la FA yaliyomalizika hivi karibuni huko Arusha, bado ana ndoto za kufanya vizuri zaidi kwenye msimu ujao.

"Malengo yangu ni kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi, nitahakikisha napambana ili nitimize malengo yangu," alisema Sopu.

Mshambuliaji huyo alisema amefurahi kuaminiwa kuitumikia Azam na amejipanga kuisaidia timu hiyo kufikia malengo yake.

"Ninawaahidi mashabiki wa Azam nitaipigania timu yangu ili tushike nafasi nzuri katika msimamo ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, pia ninaomba waendelee kuniamini," Sopu alisema.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/07/22 | 22:30 | Criciuma SC vs Vasco da Gama | 2.53 | 2.82 | 3.12 |
| 02. 10/07/22 | 00:30 | Sampaio MA vs Ituano SP | 2.47 | 2.98 | 3.03 |
| 03. 10/07/22 | 02:00 | Charlotte FC vs Nashville | 2.45 | 3.22 | 2.97 |
| 04. 10/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs New York Red Bulls | 2.92 | 3.57 | 2.31 |
| 05. 10/07/22 | 02:30 | Goias vs Atletico Pr | 2.89 | 3.08 | 2.54 |
| 06. 10/07/22 | 03:30 | Houston Dynamo vs Dallas | 2.36 | 3.47 | 2.92 |
| 07. 10/07/22 | 08:00 | Consadole Sapporo vs Kashima Antlers | 2.89 | 3.34 | 2.47 |
| 08. 10/07/22 | 13:00 | Sagan Tosu vs Kashiwa Reysol | 2.32 | 3.23 | 3.23 |
| 09. 10/07/22 | 13:00 | Omiya Ardija vs Tokyo Verdy | 2.71 | 3.32 | 2.56 |
| 10. 10/07/22 | 13:00 | Oita Trinita vs Fagiano Okayama | 2.47 | 3.00 | 3.10 |
| 11. 10/07/22 | 13:00 | Avispa Fukuoka vs Kyoto Sanga | 2.62 | 2.97 | 3.02 |
| 12. 10/07/22 | 13:00 | Suwon City vs FC Seoul | 2.90 | 3.35 | 2.42 |
| 13. 10/07/22 | 16:00 | Utsiktens BK vs Osters IF | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 14. 10/07/22 | 16:00 | Seinajoen JK vs Honka | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 15. 10/07/22 | 19:00 | Sandefjord vs Aalesunds | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 16. 10/07/22 | 02:30 | CA Platense vs Newell'S Old Boys | 2.62 | 3.07 | 2.92 |
| 17. 10/07/22 | 22:00 | Corinthians vs Flamengo | 2.73 | 3.08 | 2.68 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 08/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1039 | Sheikh Jamal vs Saif SC | 2.75 | 3.34 | 2.29 |
| 13:00 | 2124 | Mokpo City vs Changwon City | 5.10 | 3.19 | 1.70 |
| 13:00 | 5439 | Dong Tam Long AN vs DAK Lak | 2.48 | 3.10 | 2.85 |
| 13:30 | 1404 | Bentleigh Greens vs Eastern Lions SC | 1.13 | 7.07 | 13.74 |
| 13:30 | 2082 | Brisbane Roar Youth vs Peninsula Power | 5.89 | 5.50 | 1.34 |
| 13:30 | 2783 | Gangwon vs Sangju Sangmu | 2.50 | 3.09 | 2.65 |
| 13:30 | 2789 | Jeju Utd vs Seongnam Ilhwa | 1.58 | 3.70 | 5.12 |
| 14:00 | 1394 | West Adelaide W vs Salisbury Inter W | 1.49 | 4.61 | 4.71 |
| 14:00 | 1485 | Song Lam Nghe AN vs Ho Chi Minh City | 2.29 | 3.10 | 3.10 |
| 14:30 | 1152 | Guangzhou Evergrande vs Shanghai SIPG | 10.76 | 5.28 | 1.22 |
| 14:30 | 3831 | Sichuan Jiuniu vs Anhui Litian | 1.79 | 3.43 | 4.02 |
| 14:45 | 3089 | Young Lions vs Geylang Int. | 3.69 | 3.74 | 1.78 |
| 14:45 | 4210 | Albirex Niigata (SIN) vs Tanjong Pagar United FC | 1.21 | 6.29 | 8.84 |
| 16:00 | 4144 | Boca Jrs vs San Lorenzo de Almagro Res. | 1.52 | 4.03 | 5.11 |
| 16:00 | 5318 | Shakhter Karagandy vs FK Arys | 2.14 | 3.30 | 3.20 |
| 17:00 | 1692 | Puebla U20 vs Santos Laguna U20 | 3.35 | 3.50 | 2.02 |
| 17:00 | 2418 | CA Sarmiento de Junin vs Rosario Central Reserve | 2.89 | 3.24 | 2.25 |
| 17:00 | 3245 | Gimnasia de la Plata Reserve vs Atletico Tucuman Reserve | 1.85 | 3.49 | 3.68 |
| 17:00 | 5090 | Arsenal FC Reserve vs Patronato Reserve | 2.08 | 3.18 | 3.28 |
| 18:00 | 2940 | Mazatlan FC U20 vs Tigres U20 | 2.85 | 3.34 | 2.23 |
| 18:00 | 4635 | Lesotho vs Mauritius | 1.64 | 4.30 | 3.86 |
| 18:30 | 5921 | Botev Plovdiv vs Hebar Pazardzhik | 1.21 | 5.51 | 10.83 |
| 19:00 | 5698 | Spain W vs Finland W | 1.04 | 9.88 | 28.65 |
| 19:00 | 5897 | Kaisar Kyzylorda vs Akzhaiyk Uralsk | 2.42 | 3.24 | 2.65 |
| 20:00 | 5709 | FC Lokomotiv Moscow W vs FC Zenit Saint Petersburg W | 2.59 | 2.78 | 2.83 |
| 21:00 | 1162 | Harrogate vs Sheffield Wed | 3.85 | 3.85 | 1.78 |
| 21:00 | 1335 | FK Vozdovac vs Novi Pazar | 1.79 | 3.28 | 4.21 |
| 21:00 | 4881 | Albion FC vs Torque | 3.92 | 3.43 | 1.81 |
| 21:00 | 5526 | Njarovik vs IR Reykjavik | 1.45 | 4.62 | 5.11 |
| 21:00 | 5820 | Septemvri Sofia vs Ludogorets Razgrad | 10.83 | 5.51 | 1.21 |
| 21:45 | 1717 | Galway United vs Cobh Ramblers | 1.25 | 5.31 | 9.04 |
| 21:45 | 3666 | Waterford Utd vs Wexford Youths | 1.40 | 4.51 | 6.08 |
| 21:45 | 4007 | Athlone Town vs Bray Wanderers | 3.05 | 3.54 | 2.04 |
| 21:45 | 4590 | Treaty United vs Longford Town | 2.51 | 3.30 | 2.51 |
| 21:45 | 5164 | Drogheda Utd vs Dundalk FC | 4.41 | 3.62 | 1.67 |
| 21:45 | 5224 | Shelbourne vs Finn Harps | 2.03 | 3.05 | 3.59 |
| 22:00 | 4265 | Germany W vs Denmark W | 1.62 | 3.84 | 4.53 |
| 22:15 | 2707 | Aegir vs Throttur Reykjavik | 2.46 | 3.39 | 2.51 |
| 22:15 | 3589 | Haukar vs Vikingur Olafsvik | 1.84 | 3.78 | 3.44 |
| 23:45 | 4561 | America W vs Toluca W | 1.30 | 5.20 | 8.40 |

### JUMAMOSI - 09/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 3187 | Monagas SC vs Deportivo La Guaira | 2.21 | 2.99 | 3.19 |
| 00:10 | 5052 | Nueva Chicago vs Belgrano Cordoba | 3.68 | 2.84 | 2.10 |
| 01:00 | 4003 | Club Celaya vs Pumas De Tabasco | 1.66 | 3.44 | 4.82 |
| 01:00 | 4490 | CD Santa Cruz vs Santiago Morning | 2.95 | 3.15 | 2.25 |
| 01:00 | 5371 | Union San Felipe vs Copiapo | 2.30 | 3.08 | 2.94 |
| 01:00 | 5929 | Vila Nova GO vs Bahia BA | 3.13 | 2.79 | 2.37 |
| 02:00 | 1562 | Cleveland SC vs Pittsburgh Hotspurs | 2.44 | 3.58 | 2.44 |
| 02:00 | 1745 | Trinidad And Tobago W vs Costa Rica W | 8.03 | 5.09 | 1.28 |
| 02:00 | 4191 | Rosario Central vs Sarmiento Junin | 1.95 | 3.25 | 3.59 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Julai 8, 2022

Nipashe





Sterling athibitisha kuondoka City

UKURASA 21



Msanii wa kizazi kipya, Frida Amani (kushoto), akitumbuiza katika hafla maalumu iliyoandaliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ili kuwapongeza wachezaji wa Serengeti Girls ambao wamekata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za U-17 zitakazofanyika Oktoba, mwaka huu nchini India. **PICHA: IKULU**

# NABI AICHAMBUA LIGI KUU 2022/23

## Aandaa mipango mipya kukabiliana na ushindani huku akisifia nyota wapya...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha mabingwa wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Yanga kikiwa katika mapumziko, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nesredine Nabi amesema wanatakiwa kujipanga zaidi kwa sababu msimu ujao utakuwa mgumu kuliko ilivyokuwa katika msimu uliomalizika.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema amewapa wachezaji wake mapumziko ya wiki mbili na wakirejea wataanza upya kujiwinda na msimu mpya ambao pia malengo yao ni kuona wanatetea mataji yote matatu waliyoshinda.**

Nabi alisema anaamini msimu ujao ambao utaanza na mchezo wa Ngao ya Jamii, Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hautakuwa mwepesi.

Kocha huyo alisema wamejipanga kuongeza umakini na kuwaandaa wachezaji wajitume kwa sababu hakutakuwa na muda wa kujiuliza walipokosea.

"Wachezaji wamefanya kazi kubwa na nzuri msimu huu kuchukua mataji yote matatu si kazi ndogo, wanahitaji kupumzika pamoja na familia zao ikiwamo kupongezana, ila haitakuwa zaidi ya wiki mbili," alisema Nabi.

Aliongeza wachezaji wanastahili kupata muda wa kutosha zaidi, lakini muda wa likizo umekuwa mfupi kwa sababu wao pia wanashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), yapo karibu na hawahitaji kutolewa mapema.

"Wachezaji wanatakiwa kutumia vizuri huu muda wa mapumziko, nataka wakirejea kila mmoja awe makini na kufanya mazoezi, kwa sababu tutakuwa na mazoezi magumu katika siku za mwanzo za maandalizi ya msimu mpya," alisema Nabi.

Alieleza wanatarajia 'pre season' yao itaanza kwa nguvu na wachezaji watafanya mazoezi yenye kasi kubwa ili kuendelea kupata matokeo mazuri katika mashindano yote watakayoshiriki.

"Tunataka kuendelea pale tulipoishia msimu huu ambapo malengo yetu yalikuwa ni kuwapa raha mashabiki waliokuwa pamoja na timu kwa kipindi chote hadi tuliposhinda mataji matatu," Nabi alisema.

Alieleza anahitaji kuona kila mchezaji anaongeza umakini na yeye atakuwa mkali kwa nyota wake wote ili kufanikisha mipango mipya aliyoiandaa kuelekea msimu ujao unaotarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 17, mwaka huu.

Alisema amejiandaa na anafahamu mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Agosti 13, mwaka huu dhidi ya watani zao Simba ambayo ni 'Derby' ya Tanzania utakuwa mgumu, hivyo anatakiwa kuandaa taswira tofauti na iliyozoeleka.

"Kuhusu usajili sina mashaka kabisa na viongozi, matarajio makubwa ya kufanya kile nilichowaambia katika taarifa ya usajili yatatimia kwa ajili ya kuimarisha timu yetu iweze kupambana kwenye ligi ya ndani na mashindano ya kimataifa," alisema kocha huyo.

Yanga imeweka rekodi ya kumaliza msimu wa 2021/2022 bila kufungwa mechi hata moja, hivyo inataka kuona inaendeleza ubabe huo katika msimu mpya.

Ili kufikia malengo hayo, inaendelea kuimarisha kikosi chake kwa kusajili wachezaji nyota na tayari imeshamtangaza kumrejesha klabuni kwake winga wa kimataifa kutoka Ghana, Bernard Morrison aliyekuwa akiichezea Simba.

# Kichuya awaita mezani Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Namungo FC, Shiza Kichuya amesema mkataba wake na timu hiyo ya mkoani Lindi unatarajiwa kumalizika mwezi huu, lakini anaweza kubaki klabuni hapo endapo watafikia makubaliano na mabosi wake.

Baada ya kuonyesha kiwango kizuri msimu uliomalizika, Kichuya ametajwa kutakiwa na timu yake ya Simba huku Namungo bado ikiwa pia inahitaji huduma yake kwa ajili ya msimu ujao.

Kichuya alisema atakuwa tayari kumwaga wino kwa timu ambayo itakubali kumpatia kiasi cha fedha anachohitaji kwa sababu mchezo wa mpira wa miguu ndio kazi yake.

Hata hivyo Kichuya amewweka wazi hakuna kiongozi yoyote ya Simba aliyemfuata rasmi kwa ajili ya mazungumzo ya kusaini mkataba zaidi ya kuzisikia taarifa hizo kwenye baadhi ya vyombo vya habari.

"Siku zote wachezaji wanaweza kucheza popote pale kwa ajili ya kutafuta maisha na si vinginevyo. Mkataba wangu upo mbioni kumalizika mwezi huu, kama Namungo watahitaji huduma yangu na wakifika dau linalotaka basi nitasalia. Sisi wachezaji tunacheza kwa ajili ya kutafuta pesa ili tusaidie familia zetu," alisema Kichuya.

Winga huyo alisema bado ana kiwango kizuri na anaamini anaweza kutoa mchango mkubwa kwa timu itakayomsajili.

"Mashabiki wananipigia na kunikaribisha, utasikia 'karibu nyumbani', sasa mimi mtu akiniambia hivyo namuuliza anapoishi, namwambia unaishi wapi nije? Msimu ukiisha nitakuja kukutembelea, ananijibu 'simaanishi hivyo', kumbe wao wanaona kwenye vyombo vya habari kuwa eti nimesajiliwa Simba, ukweli sijawahi kupokea simu ya kiongozi yoyote wa klabu hiyo. Labda, inawezekana wakaja baadaye." Kichuya aliongeza.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >